# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

# HOTUBA YA WAZIRI WA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**MHESHIMIWA: OMAR SAID SHAABAN**

**MEI, 2021**

# YALIYOMO

1 UTANGULIZI:........................................................................1
2 MWENENDO WA BIASHARA:........................................6
2.1 Hali ya Uchumi na Biashara Duniani..............................6
2.2 Biashara baina ya Zanzibar na Jumuiya za Kikanda (EAC na SADC)......................................................7
2.3 Hali ya Biashara Zanzibar..........................................11
2.4 Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara (Inter-State Trade Balance):......................................................13
2.5 Hali ya Chakula na Bei katika Soko la Zanzibar..............14
3 HALI YA VIWANDA:..................................................17
4 UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MIPANGO YA WIZARA KWA MWAKA 2020/2021:..................................................22
4.1 Ukusanyaji wa Mapato...............................................22
4.2 Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/ 2021...24
4.3 Utekelezaji wa Malengo ya Wizara..............................25
5 CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2020/2021:..................................................65
6 PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA 2021/2022:.......67
7 SHUKRANI:...............................................................80
8 MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022:..................................................82
8.1 Mapato ya Serikali.....................................................82
8.2 Matumizi...................................................................84
9 HITIMISHO:...............................................................85
10 VIAMBATANISHO:......................................................86
Kiambatanisho namba 1:............................................86
Kiambatanisho namba 2:............................................86
Kiambatanisho namba 3:............................................87
Kiambatanisho namba 4:............................................88
Kiambatanisho namba 5:............................................89
Kiambatanisho namba 6:............................................90
Kiambatanisho namba 7:............................................91

# HOTUBA YA WAZIRI WA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA MHESHIMIWA OMAR SAID SHAABAN, KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

## KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022:

## 1 UTANGULIZI:

1. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi kwa madhumuni ya kupokea, kupitia, kuzingatia, kujadili na hatimae kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

2. **Mheshimiwa Spika,** Kwanza kabisa naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kufika katika Baraza lako hili leo tukiwa wazima na afya njema na kuendelea kutekeleza majukumu ya kujenga nchi yetu kwa usalama, amani na ufanisi mkubwa katika kipindi hiki cha awamu ya nane ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

3. **Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote, nachukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kuongoza awamu ya nane.

**Mheshimiwa Spika**, kwa heshima kubwa pia nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Watanzania tuna imani nao na matumaini makubwa katika kuendeleza nchi yetu kiuchumi na kijamii.

**4.** **Mheshimiwa Spika**, Kwa upande mwingine naomba kutoa pole kwa watanzania, kwa misiba mikubwa kwa Taifa letu kwa kuondokewa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile kwa kuondokewa na Maalim Seif Shariff Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar. Misiba hii ni pigo kubwa kwa Tanzania, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda itaendelea kuenzi michango yao katika taifa hili.

**5.** **Mheshimiwa Spika**, Pia nachukua fursa hii kuwapongeza Makamu wa kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman pamoja na Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah, kwanza kwa kuteuliwa kwao kushika nyadhifa hizi na pili kwa jitihada zao za dhati wanazozichukua za kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Vile vile kwa kutupa miongozo, maelekezo na michango katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

**6.** **Mheshimiwa Spika**, Nakuchukua fursa hii, kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Hussein

Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuniteua kuwa Waziri na kunikabidhi majukumu yanayobeba ajenda kuu ya Serikali ya Awamu ya nane ya Maendeleo ya Viwanda. Pamoja na kutambua kuwa hii ni Hotuba yangu ya Kwanza ya Bajeti nikiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, ni matumaini yangu kwamba uongozi wake imara na makini utarahisisha utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020 – 2050, pamoja na Ahadi za Chama cha Mapinduzi kupitia Ilani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2021-2025.

7. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Nane, tunatarajia mafanikio makubwa yatakayopatikana katika Sekta mbali mbali ikiwemo Sekta ya Biashara na Viwanda. Aidha, kama nitakavyoeleza katika Hotuba yangu, Serikali ya Awamu ya Nane imeweka msingi imara ya maendeleo endelevu ya Sekta za Biashara na Viwanda na pamoja na sekta nyingine kwa ujumla. Hivyo, sina budi kumshukuru kwa namna ya kipekee Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa imani yake kubwa kwangu kunikabidhi dhamana ya kuiongoza Wizara hii.

8. **Mheshimiwa Spika,** Naahidi kutumia juhudi na uwezo wangu wote alionipa Mwenyezi Mungu kutekeleza kazi na dhamana hii niliyopewa na

Mheshimiwa Rais, na ni matumaini yangu kuwa mipango tuliojipangia itatekelezwa kwa umakini na ufanisi wa juu kabisa katika uongozi wa Serikali ya Awamu hii.

9. **Mheshimiwa Spika,** Nachukua fursa hii pia kukushukuru wewe binafsi pamoja na Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa kuchaguliwa tena, pamoja na Wenyeviti wa Kamati za kudumu za Baraza bila kuwasahau wajumbe wa Kamati wa Sekta ya Kilimo, Biashara, na Utalii kwa mashirikiano makubwa mnayotupatia, ushauri na maelekezo yenu katika na kutekeleza malengo ya Wizara hii.

10. **Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya bajeti hii yamepitia katika hatua na ngazi mbali mbali za awali ikiwemo Kamati ya Uongozi ya Wizara na Kamati ya Sekta ya Kilimo, Biashara na Utalii ya Baraza la Wawakilishi. Nachukua fursa hii kuishukuru Kamati hii inayoongozwa na Mheshimiwa Ali Suleiman (Mrembo), Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele kwa kuchambua mapendekezo ya awali ya bajeti hii na hatimae kuridhia kuwasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu kwa kujadiliwa na kuidhinishwa.

11. **Mheshimiwa Spika**, Aidha, shukrani zangu za pekee zimwendee Katibu Mkuu wa Wizara hii Dkt. Islam Seif Salum kwa mashirikiano

yake makubwa anayonipatia katika kuhakikisha malengo ya Wizara yanafikiwa. Pia nawashukuru kwa dhati Wakurugenzi na viongozi wote wa Idara,Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara pamoja na wafanyakazi wote kwa juhudi zao kubwa za kuchapa kazi pamoja na mashirikiano makubwa wanayonipatia katika utekelezaji mzuri wa majukumu yangu ya kila siku.

12. **Mheshimiwa Spika,** Matayarisho ya bajeti hii yamezingatia miongozo mbali mbali iliyowekwa na Serikali ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, Ilani ya Chama cha CCM ya mwaka 2021 -2025, Maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika kipindi cha Kampeni na hotuba yake ya uzinduzi wa Baraza la kumi la Wawakilishi, Mpango wa Ukuzaji Uchumi na Kuondoa Umasikini Zanzibar, Sera za Biashara na Viwanda, maagizo yanayotolewa na viongozi wakuu wa nchi, mawazo ya wadau mbalimbali ikiwemo vingozi wa Chama cha ACT Wazalendo waliomo kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

13. **Mheshimiwa Spika**, Katika hotuba hii, nitaanza kwa kufanya mapitio ya jumla kuhusu mwenendo wa biashara na hali ya viwanda, utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2020/2021, na hatimae nitawasilisha mapendekezo ya bajeti kwa programu za Wizara kwa mwaka 2021/2022.

# 2 MWENENDO WA BIASHARA:

## 2.1 Hali ya Uchumi na Biashara Duniani

14. **Mheshimiwa Spika,** Mwenendo wa uchumi wa biashara duniani bado haujatengemaa na unaendelea kutishia kasi ya ukuaji biashara Duniani na kuathiri mchango wa sekta hii katika uchumi wa dunia (World Merchandise Trade Percentage of GDP). Katika kipindi cha mwaka 2020 mchango wa biashara duniani ulifikia Dola za kimarekani trilioni 18.8 sawa na upungufu wa asilimia 5.3 wa biashara iliyofanyika ukilinganisha na mwaka 2019 ambapo ulifikia asilimia 0.2. Kupungua huko kumetokana na kutokufanya vizuri katika biashara ya huduma, kuwepo kwa ratiba za kinga katika nchi mbalimbali, kuendelea kuwepo kwa maradhi ya Covid 19 ambayo ni tishio kubwa katika mustakabal wa biashara duniani.

15. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa taarifa ya makisio ya Shirika la Biashara la Dunia (WTO) kipindi cha mwaka 2020, usafirishaji wa bidhaa kwa nchi za Asia uliongezeka kwa asilimia 0.3 ya usafirishaji wote. Usafirishaji wa bidhaa kwa nchi za Ulaya umepungua kwa asilimia 8.0 ya usafirishaji wote. Aidha, nchi za Marekani ya Kaskazini na Marekani ya Kusini usafirishaji ulipungua na kufikia asilimia 8.5 na 4.5 ya usafirishaji wote. Nchi za Afrika nazo usafirishaji

wake umepungua hadi kufikia 8.1 ya usafirishaji wote duniani.

**16.** **Mheshimiwa Spika,** Kama nilivyoeleza hapo awali, kupungua huko kumetokana na kuwekwa kwa vizuizi vya usafiri na mikakati ya uthibiti wa Covid 19 kwa nchi zilizoendelea ikiwemo bara la Ulaya na Marekani.

## 2.2 Biashara baina ya Zanzibar na Jumuiya za Kikanda (EAC na SADC)

### Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)

- **Usafirishaji:**


**17.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2020, Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimefanya biashara kwa kusafirisha (Export) bidhaa zenye thamani ya **shilingi bilioni 65.661.** Kati ya hizo, Zanzibar imesafirisha bidhaa zenye thamani ya **shilingi milioni 628.1** ambayo ni sawa na asilimia **0.96** ya usafirshaji wote. Thamani ya usafirishaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwa mwaka 2020 imeshuka kwa asilimia **3.7** ukilinganisha na usafirishaji wa bidhaa kwa mwaka 2019. Zaidi ya asilimia 75 ya usafirishaji huo ulikwenda katika nchi ya Kenya.

- **Uagiziaji:**

**18.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha 2020,

Nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki zimeagiza (Import) bidhaa zenye thamani ya **Shilingi bilioni 847.430.** Kati ya hizo, Zanzibar imeagiza bidhaa zenye thamani ya **Shilingi bilioni 5.378** ambayo ni sawa na asilimia **0.6** ya uagiziaji wote kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, ukilinganisha na asilimia **0.5** ya uagiziaji kwa mwaka 2019. Zaidi ya asilimia 99 ya uagizaji huo ulitoka nchi ya Kenya, hivyo mdau wetu mkubwa kwa nchi za Afrika Mashariki ni Kenya na Uganda kwa asilimia ndogo sana, bado zipo fursa kwa nchi nyingine za Jumuiya. Aidha uagiziaji bidhaa unaongezeka kila mwaka ukilinganisha na usafirishaji kama inavyoonekana katika **mchoro namba 1** hapa chini.

## Mchoro Namba 1:
## Mwenendo wa Uagiziaji na Usafirishaji wa Bidhaa za Zanzibar kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (Mil.), 2016-2020




***Chanzo: Mamlaka ya Mapato – TRA, 2021***

## Jumuiya ya Nchi za Kusini Mwa Afrika (SADC)


- **Usafirishaji**

**19. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2020, Nchi za SADC zimefanya biashara kwa kusafirisha (Export) bidhaa zenye thamani ya **shilingi bilioni 65.661.** Kati ya hizo, Zanzibar imesafirisha bidhaa zenye thamani ya **shilingi milioni 799.2** ambayo ni sawa na asilimia**1.2** ya usafirishaji wote kwa Nchi za SADC. **Kiambatanisho Namba 1.**

- **Uagiziaji**

20. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa uagiziaji (Import), Nchi za SADC zimeagiza bidhaa zenye thamani ya **shilingi bilioni 847.431** kwa mwaka 2020. Kati ya hizo, Zanzibar imeagiza bidhaa zenye Thamani ya **shilingi bilioni 6.155** ambayo ni sawa na asilimia 0.7 ya uagiziaji wote kwa Nchi za SADC, uagiziaji huo ni pungufu kwa asilimia 74.2 ukilinganisha na thamani ya uagiziaji kwa mwaka 2019 ambayo ni **shilingi bilioni 23.827**. **Kiambatanisho Namba 2.**

**Mchoro Namba 2:**
**Mwenendo wa uagiziaji na usafirishaji wa bidhaa kwa Nchi za SADC (MILIONI), 2016-2020**




***Chanzo: Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, 2021***

## 2.3 Hali ya Biashara Zanzibar

### Usafirishaji na Uagiziaji wa Bidhaa:

21. **Mheshimiwa Spika,** Hali ya biashara kwa ujumla imeendelea kuimarika kwa mwaka 2020, ambapo Zanzibar imefanya biashara yenye thamani ya **Shilingi bilioni 913.09** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 803.88** mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia **13.6.** Biashara hiyo ilikuwa ni usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya Zanzibar na uagiziaji wa bidhaa kuja Zanzibar. Bidhaa zilizosafirisha nchi za nje ni pamoja na karafuu, mwani na mazao ya baharini.

22. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Zanzibar ilisafirisha nje bidhaa zenye thamani ya **Shilingi bilioni 65.66**. Kiwango hicho ni ongezeko la asilimia **35** kwa kulinganisha na usafirishaji wa bidhaa zenye thamani ya **Shilingi bilioni 48.57** kwa kipindi cha mwaka 2019. Katika usafirishaji huo, zao la karafuu lilikuwa na thamani ya **Shilingi bilioni 38.37** sawa na asilimia **58.4** ya usafirishaji wote. Nchi zinazoongoza katika kusafirisha bidhaa zetu ni India, Singapore na Dernmark.


23. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa uagiziaji bidhaa, Zanzibar iliagiza bidhaa zenye thamani ya **Shilingi bilioni 847.43** kwa mwaka 2020 ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 755.31** mwaka

2019. Bidhaa ambazo zimeagizwa kutoka nchi za nje ni pamoja na vyombo vya usafiri, mashine, bidhaa za elektroniki kama vile kompyuta, simu, bidhaa za nguo na chakula. Nchi ambazo tunaagiza bidhaa kwa wingi ni pamoja na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), China na Pakistani.

24. **Mheshimiwa Spika,** Mwenendo huu wa biashara umefanya kuongezeka kwa nakisi ya urari wa biashara kutoka **Shilingi bilioni (706.74)** hadi **Shilingi bilioni (781.77)**. Ongezeko hilo la nakisi linaonyesha kutokufanya vizuri kwa biashara kutokana na kuongezeka kwa uagiziaji wa bidhaa katika nchi yetu hasa bidhaa za mashine na vifaa vya usafiri ambavyo vina thamani kubwa. **Mchoro Namba 3** hapa chini unaonyesha hali hii

**Mchoro Namba 3:**

**<u>Mwenendo wa Biashara Zanzibar (2015 – 2020)</u>**




***Chanzo:*** **Mtakwimu Mkuu wa Serikali-OCGS, 2021**


## 2.4 Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara (Inter-State Trade Balance):

**25. Mheshimiwa Spika,** Biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara inahusisha utoaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania bara na uingizaji wa bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar. Biashara hiyo inahusisha bidhaa za vyakula vikiwemo mchele, mbatata, maharage, vitunguu, tungule, mboga mboga, viazi vitamu, matunda, vifaa vya elektroniki, magari, madawa na vinywaji.

**26. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha mwaka 2020, Zanzibar ilipeleka bidhaa Tanzania Bara zenye thamani ya **Shilingi bilioni 15.03**, ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya **Shilingi blioni 21.56** zilizopelekwa mwaka 2019. Hali hii ya kushuka imesababishwa na kupungua kwa upelekaji wa bidhaa hasa magari tokea mwaka 2016 na bidhaa zengine za viwanda zilizoshindwa kuingia katika soko hilo.

Aidha, kwa mwaka 2020, Zanzibar iliagizia kutoka Tanzania Bara bidhaa zenye thamani ya **Shilingi bilioni 243.81** ikilinganishwa na uagiziaji wa bidhaa zenye thamani ya **Shilingi bilioni 260.67** mwaka 2019**.** Kushuka kwa uagiziaji huo kumetokana na kuimarika kwa uzalishaji wa ndani kwa bidhaa chakula (mboga mboga na matunda).

**Mchoro Namba 4:**
**Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara TZS (Milioni)**




***Chanzo:*** **Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali-OCGS, 2021**

## 2.5 Hali ya Chakula na Bei katika Soko la Zanzibar

**27. Mheshimiwa Spika,** Uwepo wa chakula muhimu Zanzibar umeendelea kuridhisha. Katika kipindi cha Julai 2020 – Machi, 2021, jumla ya tani za mchele **53,594.5,** sukari tani **22,230** na unga wa ngano tani **5,390.75** ziliingizwa Zanzibar kwa ajili ya matumizi ya soko la ndani. Hata hivyo, uzalishaji wa ndani uliendelea kwa bidhaa za unga wa ngano na sukari. Takwimu zilizokusanya zinaonesha jumla ya tani 35,647 za unga wa ngano na tani 3,000 za sukari zilizalishwa nchini kwa kipindi cha Julai 2020 – Machi, 2021 **(Jadweli nambari 1)**. Kwa makisio ya sasa

ya matumizi ya bidhaa hizo, Zanzibar inatumia wastani wa tani 10,169 za Mchele, tani 3,000 Sukari na tani 3,679 Unga wa ngano kwa mwezi.

**Jadweli Namba 1:**
**Wastani wa Uingizaji wa Chakula Muhimu**
**katika Soko la Zanzibar 2020/2021 (Tani):**

| MAELEZO | Bidhaa/tani | | |
|---|---|---|---|
| | Mchele | Sukari | Unga wa ngano |
| Bidhaa zilizoingizwa Kutoka nje ya nchi (Julai 2020 - Machi 2021) | 52,037 | 22,230 | 3,345 |
| Bidhaa zilizoingizwa Kutoka T. Bara. | 1,557.5 | - | 2,045.75 |
| Bidhaa Zilizozalishwa nchini | - | 3,000 | 35,647 |
| **Jumla ya Bidhaa** | **53,594.5** | **25,230** | **41,037.75** |

***Chanzo: Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, 2021***

**28. Mheshimiwa Spika,** Mwenendo wa bei za bidhaa hizo muhimu ulionekana ukiongezeka kwa bidhaa zote za chakula. Ambapo mchele aina ya Mapembe uliongezeka kutoka TZS 1,536 hadi kufikia TZS 1,597, Unga wa ngano uliongezeka kutoka TZS 1,382 hadi TZS 1,460 na Sukari kutoka TZS 1,896 hadi TZS 1,909 kwa kipindi cha mwaka 2020/2021. Mnamo mwezi wa April 2021 Serikali iliendelea na hatua za kisera za kudhibiti bei kwa kutangaza bei elekezi kwa bidhaa hizo muhimu za chakula na bei hizo zimeonekana kuwa na utulivu katika masoko ya ndani. Kwa wastani bei za bidhaa hizo za chakula ziliendelea kuwa kama inavyoonekana katika **Jadweli Namba 2** hapa chini:

**Jadweli Namba 2:**
**Mwenendo wa Bei (Reja Reja) za Chakula kwa Kipindi cha**
**Julai 2020 – Machi, 2021**

| BIDHAA | WASTANI WA BEI (TSH) ZA REJA REJA / KG | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JUL | AUG | SEP | OKT | NOV | DIS | JAN | FEB | MACHI |
| Mchele wa Basmati /kg | 3,659 | 3,665 | 3,653 | 3,659 | 3,665 | 3,653 | 3,635 | 3,663 | 3,717 |
| Mchele aina nyengine/kg | 1,536 | 1,541 | 1,559 | 1,536 | 1,541 | 1,559 | 1,570 | 1,591 | 1,597 |
| Mchele wa Mbeya/kg | 2,133 | 2,169 | 2,191 | 2,133 | 2,169 | 2,191 | 2,095 | 2,100 | 2,074 |
| Unga wa ngano /kg | 1,382 | 1,382 | 1,382 | 1,382 | 1,382 | 1,382 | 1,415 | 1,460 | 1,460 |
| Sukari /kg | 1,896 | 1,896 | 1,896 | 1,896 | 1,896 | 1,896 | 1,902 | 1,909 | 1,909 |

***Chanzo: Wizara ya Biashara na Maendeleo ya* Viwanda, 2021**

## Mwenendo wa Mafuta ya Nishati (Fuel)

29. **Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla hali ilikua nzuri ya upatikanaji wa mafuta ya nishati kwa kipindi cha mwaka 2020/2021. Aina zote za nishati zilipatikana bila ya usumbufu kwa kipindi hicho chote. Bei za mafuta ya nishati zinaonekana katika **Jadweli namba 3.**

**Jadweli Namba 3:**

**Bei za mafuta ya nishati kwa kipindi cha 2020/2021**


| BIDHAA/ LITA | BEI (TZS) ZA MAFUTA | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JUL | AUG | SEP | OCT | NOV | DEC | JAN | FEB | MARCH |
| Petrol | 1,751 | 1,884 | 1,907 | 1,918 | 1,948 | 1,912 | 1,882 | 1,934 | 2026 |
| Diesel | 1,856 | 1,925 | 1,931 | 1,901 | 1,866 | 1,820 | 1,829 | 1,960 | 2041 |
| Kerosene | 1,800 | 1,188 | 1,308 | 1,606 | 1,606 | 1,233 | 1,261 | 1,376 | 1,471 |

***Chanzo: Wizara ya Biashara na Maendeleo ya* Viwanda, 2021**

# 3 HALI YA VIWANDA:

**30.** **Mheshimiwa Spika,** Asilimia kubwa ya nchi zilizoendelea dunia zimetokana na uchumi imara wa Sekta ya Viwanda, ambao hutumika kupima maendeleo ya nchi kwa kuzingatia mchango wake katika Pato la Taifa. Mheshimiwa Spika, Mchango wa Viwanda katika pato la Taifa umeendelea kuongezeka kutoka asilimia 18.3 mwaka 2019 hadi kufikia asilimia 19.6 mwaka 2020. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 1.3 kutokana na kuimarika kwa sekta uzalishaji Viwandani. Ongezeko hili la asilimia 0.9 limechangiwa na kuongezeka kwa sekta ya ujenzi asilimia 8.9 kwa mwaka 2020 ukilinganisha na asilimia 8.6 kwa mwaka 2019. Ambapo sekta ya uchimbaji imepungua kufikia asilimia 1.0 mwaka 2020 kulingana na asilimia 1.1 mwaka 2019.

**Mchoro Namba 5:**




***Chanzo: Wizara ya Biashara na Maendeleo ya*** **Viwanda, 2021**

**31. Mheshimiwa Spika,** Hali ya uzalishaji bidhaa viwandani kwa mwaka 2020/2021 inaendelea kuimarika licha ya kuwepo kwa changamoto ya ushindani wa soko kwa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje. Kiwanda cha maziwa cha ADPL chenye uwezo wa kuzalisha lita 64,800,000 kwa mwaka na kimeajiri wafanyakazi 67, kimeweza kuzalisha lita 3,600,000 za maziwa hadi kufikia Machi 2021 sawa na asilimia 5 ya uwezo wake. Kwa kipindi cha miaka miwili ya uzalishaji imekuwa ya hasara kutokana na kuongezeka kwa tozo ya bidhaa za mifugo ikiwemo maziwa kutoka TZS 150 kwa lita moja hadi TZS 2,000 kwa lita moja na kuanzia mwezi Agosti,2018. Hata hivyo Wizara iliendelea kufanya majadiliano na Mamlaka za Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano wa karibu na ADPL, hatimae kufanikiwa kuishusha tozo hiyo hadi kufikia TZS 250 kwa lita moja. Aidha, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo nayo iliandaa kanuni ya tozo ya TZS 250 kwa maziwa yanayoingia kwenye soko la Zanzibar kutoka Tanzania Bara na TZS 1,000 kwa maziwa yanayotoka nje ya Tanzania kwa lengo la kuweka ushindani halali katika soko.

**32.** **Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha Zanzibar Milling Corporation (ZMCL) kilichopo Mtoni kinachozalisha bidhaa ya unga wa ngano chenye uwezo wa kuzalisha tani 64,800 na kuajiri wafanyakazi 110 kimeendelea kuimarika kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji. Hadi kufikia Machi 2021 jumla ya tani 62,300za unga wa ngano sawa na asilimia 96 ya uwezo wa Kiwanda zimeweza kuzalishwa. Kwa sasa kinaendelea na upanuzi wa eneo la uzalishaji na uhifadhi.

**33.** **Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha Sukari (ZSFL) kilichopo Mahonda hadi kufikia Machi, 2020/2021 kimezalisha jumla ya tani 3,000 za sukari. Aidha, juhudi za kupatikana maeneo zaidi ya kuongeza kilimo cha miwa zinaendelea kwa ushirikiano mkubwa baina ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, (AR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na

Mifugo, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi. Kupatikana kwa maeneo mapya ya kilimo cha miwa kutapelekea kupatikana kwa malighafi ya kutosha kuzalisha tani 8,000 za sukari, lita 800,000 za spiriti na tani 4,500 za molasses. Kwa sasa Kiwanda kinakabiliwa na changamoto ya maeneo zaidi waliyoyahitaji kama walivyoahidiwa

**34.** **Mheshimiwa Spika**, Vipo viwanda kadhaa ambavyo vinaendelea na uzalishaji. Miongoni mwa viwanda hivyo ni Turky Mifuko kinachozalisha mifuko (carrier bags) kilichopo Mgeni Haji chenye uwezo wa kuzalisha kilo 500,000 za mifuko kwa mwezi, Kiwanda kipya cha Zanto cha kusarifu tungule (Tomato Paste) na pili pili (Chilli Sauce) kilichopo Shakani, Kiwanda cha kuzalisha vifungashio (Messab Packaging) kilichopo Dimani, Kiwanda cha kusarifu zao la chumvi kilichopo Kiembe Samaki, Kiwanda cha kuzalisha mafuta ya nazi (Virgin Coconut Oil), Kiwanda cha kutengeneza mabati, Kiwanda cha kubangulia korosho na Kiwanda cha kuzalisha vifungashio vya kuhifadhia vyakula vilivyopo katika Eneo la Viwanda Amani.

**35.** **Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha Basra Textiles Mills Co. Limited cha nguo kimeanza uzalishaji ingawa kilipata changamoto wakati wa shehena ya mzigo wao ulipoingia bandari ya Dar-es-Salaam kwa kutakiwa kulipa ushuru wa forodha

kwa vile kodi hiyo haikulipwa wakati wa uingizaji wa mali ghafi (Grey fabric). Hata hivyo baada ya majadiliano na TRA – Dar-es-Salaam changamoto hiyo imemalizika baada ya Kiwanda cha BASRA kulipa ushuru wa forodha hapa Zanzibar.

36. **Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha kusarifu zao la mwani – Chamanangwe Pemba ambapo kazi ya ujenzi wa kiwanda unaendelea ikiwa ni katika hatua za kukamilisha ramani na makisio ya ununuzi ya vifaa vya ujenzi. Kazi hii inafanywa kwa ushirikiano kati ya ZSTC na Kampuni ya Ocean fresh na Kappa Carrageenan Nusantara za nchini Indonesia. Uwezo wa kiwanda unatarajiwa kuzalisha kilo 240 za bidhaa ya agar agar na kilo 378 kwa bidhaa ya carragena kwa mwaka. Kiwanda hicho kinatarajia kuwa na uwezo wa kusarifu tani 30,000 kwa mwaka.

37. **Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha kusarifu zao la chumvi – Chamanangwe Pemba, Kampuni ya Zanzibar Coast Salt Company Limited kinaendelea na kuzalisha bidhaa ya chumvi za aina nane kwa matumizi mbali mbali na kuuza katika masoko yetu ya ndani ikiwemo utalii. Aidha, eneo la ujenzi wa kiwanda hicho (site plan) tayari limeshatengwa katika eneo la Chamanangwe. Wakati mpango mkakati wa kuongeza uzalishaji chumvi ili kukidhi mahitaji ya kiwanda ukiendelea. Kumejitokeza changamoto

ya eneo la uzalishaji chumvi la AZASPO ambalo wazalishaji wametakiwa kuondoka na badala yake eneo hilo linatakiwa kutumika kwa shughuli nyingine za taasisi ya serikali.

38. **Mheshimiwa Spika,** Viwanda vilivyoanzishwa na kufanya kazi ni pamoja na viwanda vya mafuta ya kupikia ya alizeti, viwanda vya Tungule, Mafuta ya Nazi, Mifuko ya kufungashia, Misumari, kusarifu mwani, Maziwa, Chumvi, Paipu za mifereji na Mafuta ya majani ya Karafuu. Viwanda hivi vitaongeza upatikanaji wa bidhaa, ajira, na Pato la Taifa.

39. **Mheshimiwa Spika,** baada ya shukrani na maelezo hayo ya awali kuhusu hali ya biashara na viwanda, naomba sasa niwasilishe utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na mwelekeo wa malengo ya mwaka 2021/2022.

# 4 UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MIPANGO YA WIZARA KWA MWAKA 2020/2021:

## 4.1 Ukusanyaji wa Mapato

40. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara Biashara ilipangiwa lengo la kukusanya mapato ya **shilingi bilioni 2.368** kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali. Hadi

kufikia mwezi wa Machi, 2021, jumla ya **Shilingi bilioni 1.068** zilikusanywa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambapo ni sawa na asilimia **60.5** ya makadirio ya makusanyo kwa kipindi cha miezi tisa (Julai – Machi ya shilingi bilioni 1.766). Kiasi hicho cha makusanyo pia ni sawa na asilimia **45** ya makisio ya makusanyo ya mwaka wa fedha 2020 /2021.

**41.** **Mheshimiwa Spika,** Sababu ya kushuka kwa mapato imetokana na ugonjwa wa Covid 19 ambapo biashara na uzalishaji kwa jumla viliathirika. Aidha ukosefu wa vitendea kazi kwa baadhi ya taasisi zetu ambazo ni mpya pamoja na upatikanaji wa mdogo wa bajeti umechangia ukusanyaji mdogo wa mapato.

**42.** **Mheshimiwa Spika,** Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi milioni 80.301 zilipangwa kukusanywa kwa upande wa Ofisi kuu Pemba, hadi kufikia 31 Machi, 2021 jumla ya shilingi milioni 34.421 zimekusanywa ikiwa ni sawa na asilimia **43** ya fedha zilizopangwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha.

Kwa upande wa Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko kupitia kitengo cha Vipimo na Mezani, kilipanga kukusanya Shilingi milioni 154.400 hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2021 jumla ya shilingi milioni 64.210,zimekusanywa sawa na

asilimia 42 ya makadirio ya mapato kwa mwaka. Kwa upande wa malipo ya kazi za biashara na ukodishwaji wa maeneo ya kibiashara, Wizara ilipanga kukusanya shilingi milioni 447.268, hadi kufikia Machi, zimekusanya shilingi 86.644 sawa na asilimia 19.

Aidha, Taasisi ya Viwango (ZBS) ilipangiwa kukusanya Shilingi milioni 976.000 kutoka katika malipo ya usimamizi wa viwango, hadi kufikia 31 Machi, 2021 jumla ya Shilingi milioni **175.000** zimekusanywa sawa na asilimia 18 ya mapato kwa kipindi hiki.

Kadhalika, Wakala wa Usajili Biashara na Mali (BPRA) ilipanga kukusanya Shilingi milioni 709.827 kutokana na vyanzo vyake mbali mbali vya mapato kwa huduma inazotoa, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2021 jumla ya Shilingi milioni 707.821 sawa na asilimia 100 zimekusanywa kwa kipindi hiki.

**43.** **Mheshimiwa Spika,** Mchanganuo wa Mapato hayo kwa kipindi cha Julai 2020 - Machi 2021 ni kama unavyoonekana katika **Kiambatanisho Namba 3.**

## 4.2 Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/ 2021

**44.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Biashara na Maendeleo

ya Viwanda, iliidhinishiwa matumizi ya jumla ya **shilingi bilioni 23.570** kwa ajili ya kutekeleza program zake. Kati ya hizo **shilingi bilioni 8.77** kwa ajili ya kazi za kawaida na **shilingi bilioni 14.80** kwa kazi za maendeleo ikiwemo **shilingi bilioni 4.6** kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya wazalishaji wadogo wadogo na wa kati Khalifa Fund. Hadi kufikia Machi 2021, Wizara iliingiziwa jumla ya **shilingi bilioni 4.41** sawa na asilimia **23** ya bajeti ya miezi tisa (ya Shilingi bilioni 19.50) ambazo ni sawa na asilimia **19** ya bajeti ya mwaka. Mchanganuo wa matumizi hayo kwa kila program ulikuwa kama unavyoonekana katika **Kiambatanisho Namba 4.**

## 4.3 Utekelezaji wa Malengo ya Wizara

**45. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ulifanyika kulingana na huduma na shughuli zilizowekwa katika programu kuu Nne za Wizara kama ifuatavyo:

### PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA BIASHARA NA VIWANDA

**46. Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Viwanda imeundwa na Programu ndogo tatu ambazo ni Utawala na Uendeshaji wa Wizara;

Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti; na Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba. Katika kutekeleza majukumu yake, program hii ilipangiwa matumizi ya **shilingi bilioni 3.53** kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba, hadi kufikia Machi 2021, programu hii imeingiziwa jumla ya **shilingi bilioni 1.633** ikiwemo mishahara na kazi nyengine za uendeshaji sawa na asilimia **59** ya fedha zilizopangwa kwa miezi tisa ambazo ni sawa na asilimia **46** ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa huduma zilizopangwa katika kila program ndogo nilizozitaja ni kama ifuatavyo:

**Programu ndogo ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara:**

**47.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Huduma zinazotolewa katika programu hii ndogo ni pamoja na huduma ya ununuzi wa vifaa vya ofisi na usafiri, huduma ya usimamizi wa rasilimali watu na huduma kwa ujumla pamoja na kuratibu mikutano ya majadiliano ya kibiashara na viwanda ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Program hii ndogo ilipangiwa matumizi ya **shilingi bilioni 2.29** kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia Machi 2021, programu

hii ndogo imeingiziwa jumla ya **shilingi bilioni 1.04** ikiwemo mishahara na kazi nyengine za uendeshaji sawa na asilimia **45** ya makadirio ya mwaka. Huduma za Program ndogo ya Utawala na Uendeshaji zilitekelezwa kama ifuatavyo:-

**Usimamizi wa Rasilimali Watu na Huduma kwa Ujumla:**

48. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2020/2021 Wizara imeanza kufanya zoezi la tathmini ya kiutendaji kwa wafanyakazi wake (Performance Appraisal) na kuwapatia nyongeza wafanyakazi kwa kuzingatia muongozo wa Utumishi wa Umma Serikalini pamoja na kuwalipa mishahara wafanyakazi. Wafanyakazi 69 wamepatiwa likizo, kati ya hao wafanyakazi 35 likizo la kawaida, 22 likizo la dharura na 12 likizo la uzazi. Vile vile wafanyakazi 3 wamepatiwa huduma ya mazishi na wafanyakazi 2 wamestaafu kazi kwa hiari.

49. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuwajengea uwezo watumishi wake, Wizara kwa mwaka 2020/2021 imeendelea kutekeleza Mpango wa mafunzo kwa kumpatia mafunzo ya muda mrefu mfanyakazi mmoja katika ngazi ya shahada ya kwanza fani ya uchumi, pamoja na kuwapatia mafunzo elekezi ya kiutendaji serikalini wafanyakazi 18. Aidha, jumla ya wafanyakazi 4 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbalimbali

vya ndani na nje ya nchi. Kati ya hao watumishi 2 wanashiriki shahada ya Uzamivu, mtumishi 1 anashiriki shahada ya Uzamili katika fani ya Uchumi, na mtumishi 1 anashiriki shahada ya kwanza ya katibu muhtasi. Vile vile wafanyakazi 3 wamepandishwa vyeo baada ya kurudi masomoni, mtumishi 1 amehitimu shahada ya kwanza katika fani ya Uhandisi na watumishi 2 shahada ya Uzamili, 1 fani ya Utawala na mwengine fani ya Takwimu.

**Kadhalika,** Katika mwaka 2020/2021 Wizara imefanya ukarabati wa majengo mawili ya Ofisi kwa lengo la kuimarisha mazingira mazuri ya kiutendaji. Jengo la makao makuu lililopo Malindi limafanyiwa ukarabati wa ofisi za viongozi na vyoo na jengo la Ofisi Darajani limefanyiwa ukarabati kwa kupakwa rangi.

**50.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Wizara imefanikiwa kufanya kikao kimoja cha Wafanyakazi katika masuala ya Rushwa, UKIMWI na Jinsia. Kupitia kikao hicho elimu imetolewa kwa watumishi juu ya athari ya vitendo visivyo na uadilifu kazini vikiwemo rushwa, pamoja na kuzingatia sheria, kanuni na mkataba wa huduma wa Wizara wakati wa kutoa huduma. Jitihada za kupambana na kujikinga na maambukizi ya UKIMWI pamoja na kuzingatia masuala ya jinsia katika sehemu zote za kazi.

### Huduma ya Ununuzi wa Vifaa vya Ofisi

51. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2020/2021 upatikanaji wa huduma za Ofisi kwa wakati zimeendelea kuimarika kutokana na uzingatiaji wa Mpango wa Ununuzi wa mwaka. Ununuzi uliofanyika katika kipindi hicho ni pamoja na vifaa vya kuandikia, mafuta, vifaa vya usafiri, Kompyuta na vifaa vyake na vifaa vya usafiri.

### Uratibu wa Mikutano ya Majadiliano ya Kibiashara na Viwanda ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa

52. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kufanya juhudi mbalimbali ili kuimarisha matumizi ya fursa za biashara na viwanda zinazopatikana na kutafuta fursa nyingine kupitia majadiliano hayo. Kwa kufanya hivyo, Wizara imeratibu na kushiriki mikutano 5 ya Kikanda, Kitaifa na Kimataifa ikiwemo ushiriki wa Baraza la Biashara wa EAC, mkutano maalum baina ya Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda na Waziri wa Viwanda na Biashara wa Tanzania bara. Ambao ulijikita zaidi katika kutafuta suluhisho ya changamoto za kibiashara zilizopo.

## Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

53. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha Wizara inaimarisha ukusanyaji wa mapato, matumizi na usimamizi sahihi wa rasilimali nyengine zisizo za kifedha za Serikali, Wizara katika kipindi hicho

imepanga kufanya ukaguzi wa kifedha, rasilimali watu, rasilimali za kudumu pamoja na ununuzi na uondoshaji wa mali za Wizara ili kuhakikisha kwamba Sheria, Kanuni, miongozo na taratibu zilizowekwa zinafuatwa. Aidha, katika kutimiza malengo hayo Kitengo cha Ukaguzi cha Wizara kimefanya kaguzi tatu ambazo ni Ukaguzi wa Ndani wa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa Wizara na Taasisi zake, Ukaguzi unaohusiana na utekelezaji wa Mpango kazi wa Wizara kwa kipindi cha Julai-Septemba na Oktoba –Disemba kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na ukaguzi unaohusiana na kuimarisha mapato na matumizi kwa Taasisi zilizo ndani ya Wizara kwa kipindi cha Julai-Septemba na Oktoba-Disemba kwa mwaka 2020/2021.

54. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa vikao vya Kamati ya Ukaguzi, Wizara katika kipindi hicho imefanya vikao 3, kati ya hivyo, vikao viwili vimejadili ripoti zilizowasilishwa na Mkaguzi wa Ndani na wa Nje kulingana na kaguzi zilizofanywa na kikao kimoja cha Kamati ya Ukaguzi kimejadili ripoti ya ufungaji wa hesabu "Final Account" 2019/2020, Mpango Kazi wa Ukaguzi wa Ndani kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Mpango kazi wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na Ripoti ya Kamati ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, ushauri ulitolewa na Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani pamoja na Kamati

ya Ukaguzi umefanyiwa kazi na Wizara hali ya udhibiti imeimarika katika ukusanyaji wa mapato, matumizi na usimamizi bora katika rasilimali zisizo za kifedha za Wizara.

## Kitengo cha Huduma za Sheria

55. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara kwa kushirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanya tafsiri ya kanuni tatu "The Zanzibar Standards (Tested Products) Regulations of 2014, "The Standards (Certification) Regulation of 2014 na The Zanzibar Standards (Compulsory batch certification of imports) regulation, of 2014. Lengo ni kuhakikisha uwepo na uwelewa wa pamoja wa Kanuni hizo kwa watumiaji. Pamoja na kukamilisha uandaaji wa Sheria Namba 6 ya mwaka 2020 ya Vipimo (Zanzibar Weight and Measure Act Nam. 6 of 2020) ambayo imepitishwa na Baraza lako tukufu na kuundwa kwa Taasisi inayoisimamia. Vile vile, Wizara imefanya mapitio ya sheria na kanuni za biashara kwa lengo la kuweka utaratibu mzuri wa usimamizi wa maswala ya biashara nchini.

## Kitengo cha Hesabu na Udhibiti wa fedha

56. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa kitengo cha hesabu na uthibiti wa fedha cha Wizara kimekamilisha uandaaji wa taarifa za utekelezaji mapato na matumizi ya fedha ya kila robo mwaka pamoja na taarifa ya mwaka.

### Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara

**57. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Programu hii ndogo imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kutayarisha, kuchambua na kutathmini utekelezaji wa mipango na malengo maalum ya Wizara. Huduma ambazo zimesimamiwa na Programu hii ndogo ni Uandaaji na Uibuaji wa Sera na Tafiti za Wizara, Uandaaji na Utekelezaji wa Mipango ya Wizara na Usimamizi wa Takwimu za Biashara na Viwanda. Program hii ndogo ilipangiwa matumizi ya **shilingi milioni 579.08** kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia Machi 2021, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya **shilingi milioni 225.50** ikiwemo mishahara na kazi nyengine za uendeshaji sawa na asilimia **39** ya makadirio ya mwaka.

### Uandaaji na Uibuaji wa Sera na Tafiti za Wizara

**58. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhakikisha uwepo wa mazingira mazuri ya ufanyaji biashara, ambapo kwa sasa imekamilisha kufanya tafsiri ya Kiswahili na kuchapisha Sera ya Maendeleo ya Sekta Binafsi ya mwaka 2020. Ni matarajio yangu kwamba, Sera hii itasaidia katika kuongeza msukumo zaidi wa uwekezaji

na kuhakikisha uzingatiaji wa ushirikishwaji wa Sekta binafsi ambao utaboresha mazingira mazuri ya biashara.

Aidha, Wizara imekamilisha rasimu ya Sera ya Biashara na kuiwasilisha kwa wadau, Sera hii inatarajiwa kukamilika mwaka ujao wa fedha.

**59.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Utalii na Mambo ya kale, Wizara ya Kilimo na Maliasili zisizorejesheka na Wizara ya Afya wamekamilisha rasimu ya utafiti wa mimea na bidhaa tiba ambao utakuwa ni chachu ya kuendelea na programu ya "Wellness". Tafiti hiyo imeweza kuainisha mimea tiba ambayo inaweza kutumika katika kutengeneza nyungu yenye sura ya upekee kwa kuzingatia tamaduni na itikadi za wananchi wa Zanzibar kwa lengo la kukuza utalii wetu. Lengo ni kuweza kupunguza kuingiza bidhaa ambazo zinahatarisha afya ya Wazanzibari.

**60.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kuendeleza Uwanja wa Maonesho wa Kimataifa Zanzibar, Wizara imekamilisha ripoti ya awali ya mazingira (Scoping) ya Uwanja wa Maonesho pamoja na kutoa uelewa kwa jamii (Community engagement) wa ujenzi huo kwa wanajamii wanaoishi katika eneo la mradi. Hii ni kutokana kwamba mradi huu kwa sasa umewekwa katika sura ya miradi ya mashirikiano baina ya Serikali na Sekta binafsi.

## Uandaaji na Utekelezaji wa Mipango ya Wizara

61. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha utekelezaji wa malengo ya Wizara tuliopanga kwa mwaka wa fedha 2020/2021 yamefikiwa, Wizara imeandaa rasimu ya Mpango Mkakati wa Wizara wa mwaka 2021-2025 pamoja na kutoa uelewa wa uzingatiaji wa muongozo mpya wa Mpango Mkakati (Score Card) kwa taasisi na Idara zilizopo chini ya Wizara hii. Aidha, ripoti za utekelezaji wa miradi na kazi za kawaida kwa kila kipindi cha robo mwaka zimeandaliwa pamoja na kuandaa vipaumbele kwa sekta ya Biashara na Viwanda kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

## Usimamizi wa Takwimu za Biashara

62. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara imeweza kutatua changamoto zilizokuwa zikijitokeza katika uhifadhi wa takwimu za biashara na viwanda kwa kuanzisha Kanzi data ya taarifa za takwimu hizo. Kwa sasa Kanzi data hiyo ya takwimu ipo katika hatua za majaribio. Aidha taarifa za takwimu za Biashara na Viwanda kwa robo mwaka zimeandaliwa na kuwasilishwa kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa hatua zinazofuata. Vile vile Wizara imefanikiwa kupata ofisi katika eneo la bandarini ili kurahisisha upatikanaji wa takwimu kwa uhakika.

### Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba

63. **Mheshimiwa Spika**, Programu ndogo ya Ofisi Kuu Pemba ina jukumu la kutekeleza na kusimamia shughuli zote za Wizara ya Biashara na Viwanda kwa upande wa Pemba. Program hii ndogo ilipangiwa matumizi ya **shilingi milioni 652.94** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, na hadi kufikia Machi 2021, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya **shilingi milioni 372.63** ikiwa ni mishahara na kazi nyengine za kawaida sawa na **asilimia 60** ya makadirio ya mwaka. Huduma iliyopangwa kutolewa na Programu hii imetekelezwa kama ifuatavyo:-

### Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba

64. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza huduma hii, Wizara ilifanya shughuli mbali mbali zikiwemo;

   i. Utoaji wa huduma na ununuzi wa vifaa ambapo Wizara kupitia Afisi Kuu Pemba ilifanya ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi, ununuzi wa huduma za umeme, maji na mawasiliano, kufanya matengenezo ya magari, ununuzi wa–mafuta na kutoa huduma ya usafiri kwa maafisa wa Wizara kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi mbali mbali za wizara;

ii. Usimamizi rasilimali watu na huduma kwa ujumla katika kuhakikisha wafanyakazi wanapatiwa stahiki zao, Wizara kupitia ofisi kuu Pemba imewapatia mafunzo ya awali wafanyakazi wapya (4) juu ya namna ya kujua Sheria za Utumishi katika kutekeleza majukumu yao. Aidha Wizara imewapatia Wafanyakazi watano (5) stahiki zao za likizo;

iii. Katika hatua ya kuwakuza na kuwaendeleza Wajasiriamali Wizara ilitembelea jumla ya vikundi 104 vya Wajasiriamali na kuandaa mikutano mitatu (3) ili kusikiliza changamoto zao na kuweza kuzitatua katika Wilaya zote za Pemba. Kati ya vikundi hivo, Nane (8) vilishiriki katika maonesho ya Viwanda Dar-es-Salam, vikundi kumi (10) vilipelekwa Tanga kujifunza kivitendo na vikundi kumi na sita (16) vilishiriki katika maonesho ya saba saba Tanzania Bara na kimoja (1) kushiriki Tamasha la Biashara la Zanzibar.

iv. Katika hatua ya kumlinda mtumiaji, Wizara ilifanya ukaguzi wa mizani na vipimo kwa mujibu wa Sheria. Katika ukaguzi huo, jumla ya mizani 576, mita ndogo za mafuta 45, magari 6 ya kubebea

mafuta na matangi 3 ya mafuta ya chini yamekaguliwa katika shehia mbali mbali za Wilaya zote za Pemba. Aidha, Wizara ilifanya ukaguzi wa maduka, maghala na bekari kwa mujibu wa Sheria ya Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji Nam 5 ya mwaka 2018. Katika ukaguzi huo jumla ya maduka 1,468 maghala 27 na bekari 45 zimekaguliwa.

v. Kusimamia bei za bidhaa muhimu katika soko la Pemba, ambapo ziliendelea kuonekana katika hali ya wastani kiasi ambacho Wananchi wa Kisiwa hicho hazikuweza kuwaathiri katika ununuzi wa bidhaa hizo, ingawa katika kipindi cha Octoba mpaka Disemba bei zilipanda kutokana na mabadiliko ya Dola ya marekani kupanda na msimu mdogo wa mavuno katika nchi tunazonunua bidhaa hizo.

   Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Serikali inaendelea na utaratibu wa kusimamia na kudhibiti bei za bidhaa muhimu kama Sheria ya Biashara nambari 14 ya mwaka 2013 inavyotutaka.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI

**65. Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Maendeleo ya Viwanda ambayo utekelezaji wake unasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Wakala wa Maendeleo ya Viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati (SMIDA) inajumuisha Programu ndogo mbili ambazo ni Ukuzaji Viwanda na Maendeleo ya Wajasiriamali. Program hii kuu ilipangiwa jumla ya **shilingi bilioni 12.78** kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia Machi 2021, programu hii kuu imeingiziwa jumla ya **shilingi milioni 836.40** ikiwemo mishahara, kazi za maendeleo na kazi nyengine za kawaida, sawa na asilimia **8** ya fedha zilizopangwa kwa robo tatu pia ni sawa na **asilimia 7** ya makadirio ya mwaka. Program ndogo hizo utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

### Programu Ndogo ya Ukuzaji Viwanda

**66. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Ukuzaji Viwanda ina jukumu la kutoa huduma ya kuimarisha sekta ya viwanda. Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya **shilingi bilioni 3.61** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, na hadi kufikia Machi 2021, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya **shilingi Milioni 811.24** ikiwemo mishahara, kazi za maendeleo na kazi nyengine

za kawaida, sawa na **asilimia 22** ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa program ndogo ya Ukuzaji Viwanda ulikuwa kama ifuatavyo:-

### Uimarishaji wa Sekta ya Viwanda

**67. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na mpango wake wa kurahisisha na kuweka mazingira mazuri ya uekezaji katika sekta ya viwanda. Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Wizara imekamilisha ujenzi wa barabara katika eneo la viwanda la Chamanangwe pamoja na upelekaji wa huduma ya umeme na maji. Kwa upande wa Unguja, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi inaendelea na kazi ya kulipima eneo la viwanda Dunga Kiembeni pamoja na kuandaa hadidu rejea kwa ajili ya kumtafuta Mshauri elekezi wa kuandaa mpango mkuu wa viwanda katika eneo hilo (Industrial Master Plan). Aidha, Wizara kwa ushirikiano na Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imekamilisha kazi ya kufanya tathmini ya katika eneo lililotengwa kwaajili ya viwanda huko Nungwi kwa lengo la kulipa fidia kwa wananchi watakaoathirika na mpango huo. Aidha Wizara pia kwa ushirikiano na ZECO pamoja na ZAWA inaendelea na kazi ya kufanya tathmini ya gharama za kupeleka miundombinu ya umeme na maji.

**Kadhalika,** Wizara yangu imefanya utafiti mdogo wenye lengo la kuangalia gharama za nishati ya uzalishaji katika viwanda vyetu nchini na taarifa inayohusiana na gharama hizo imekamilika. **Kiambatanisho namba 5** kinafafanua mlinganisho wa viwango na bei za kuuzia umeme baina ya ZECO kwa upande wa Zanzibar na TANESCO kwa upande wa Tanzania bara.

Aidha, ripoti ya awali (Scoping) kuhusu uwezekano wa kuanzisha viwanda vya kusarifu matunda Chamanangwe imeandaliwa na kazi hiyo inatarajiwa kuendelezwa katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022

68. **Mheshimiwa Spika**, Katika kutambua umuhimu wa zao la mwani katika uchumi wa taifa, Wizara inaendelea na uratibu wa uanzishwaji wa Kiwanda cha mwani kinachotarajiwa kujengwa katika eneo la Viwanda Chamanangwe Mkoa wa Kaskazini Pemba. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wataalam kutoka Indonesia wamekamilisha michoro ya ujenzi huo ambayo imewasilishwa kwa Wakala wa Majengo (ZBA) ili kuiweka sawa kiitalaam.

69. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha mnyororo wa thamani wa zao la mwani; Wizara kwa ushirikiano na REPOA iliandaa mafunzo na kutoa vifaa kwa ajili ya kulima mwani katika

kina kirefu cha maji. Mafunzo hayo yalifanyika tarehe 14/12/2020 hadi tarehe 22/12/2020 na kuwashirikisha wakulima 66 katika kijiji cha Chokocho, Tumbe na Makangale ambapo jumla ya tani mbili za mwani aina ya kotonii ulivunwa kwa kipindi cha siku 45 za mwanzo baada ya mafunzo hayo.

**70.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kushirikiana na UNIDO kwa kuwajengea uwezo wataalamu wa ndani. Jumla ya wataalamu kumi wa kitengo cha Intelijensia ya Viwanda walipatiwa mafunzo kuhusu kuendeleza mnyororo wa thamani (value chains) wa bidhaa za viungo, matunda na mboga mboga.

**71.** **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo vidogo na vya Kati (SMIDA), anajukumu la kuwaweka pamoja Wazalishaji wadogo na wa kati na kuwajengea mazingira wezeshi ya kuzalisha bidhaa zenye ubora na zenye kuweza kushindana katika masoko ya ndani, Kanda na Kimataifa. Kuzalisha ajira, kupunguza umasikini pamoja na kuongeza mchango wa sekta ya viwanda vidogo na vya kati katika Pato la Taifa.

**72.** **Mheshimiwa Spika,** Wakala imewapatia mafunzo Wajasiriamali 280 Unguja na Pemba juu ya utengenezaji wa bidhaa za matunda na Mboga

mboga, utengenezaji sabuni, utengenezaji wa mbolea kwa kutumia mwani pamoja na uandishi wa miradi na michanganuo ya kibiashara. Aidha, jumla ya Wabunifu 20 wamesaidiwa kuendeleza bunifu zao na Mbunifu mmoja anaendelezwa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na Wakala imeingia makubaliano na Mbunifu wa mashine za mwani ili kuweza kutengeneza mashine hizo kwa wingi zaidi.

**73.** **Mheshimiwa Spika,** SMIDA iliandaa uzalishaji wa mbolea kwa kutumia mwani, ambapo majaribio ya mbolea hiyo yamefanyika katika maeneo ya Kizimbani, katika mashamba ya miwa na mpunga. Aidha sampuli ya mbolea hiyo pia ilipelekwa Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA) kwa ajili ya uchunguzi zaidi. Hivyo kwa sasa SMIDA inaandaa matayarisho ya kuanza uzalishaji wa mbolea hiyo kwa ajili ya biashara.

**Aidha,** SMIDA imefanya uchambuzi wa miradi na kwa sasa miradi 13 imechapishwa katika tovuti (website) ya UNIDO kwa ajili ya kutafuta wafadhili na wadau wa biashara kwa utekelezaji. Wizara kupitia SMIDA imeandaa MoU ya mashirikiano baina ya Wizara na TAHA yenye lengo la kujenga eneo la pamoja la kusarifu viungo (spices processing facility hub) kwa sasa inatarajiwa kuwasilishwa Wizarani kwa lengo la maboresho zaidi.

**74. Mheshimiwa Spika,** Wakala imekamilisha maandalizi yote ya mradi wa kuliongezea thamani zao la dagaa nyaraka za Mpango wa biashara, ramani na michoro ya hati za zabuni zimekamilika. Mara baada ya mchakato wa kupitishwa mradi huo kukamilika, Wakala itaanza utekelezaji wake mara moja katika diko la Fungurefu Mkokotoni Mkoa Kaskazini Unguja. Aidha, Wakala imekamilisha rasimu ya hati ya makubaliano baina ya ZSSF na TAHA rasimu hizo zitapitiwa na pande zote mbili kabla ya kuanza utekelezaji wake Aidha, Wakala wameingia makubaliano na jumuiya ya Pemba Community Forest kwa ajili ya uendeshaji wa kituo chake cha Pujini Pemba kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa Wajasiriamali.

**75. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeanza ujenzi wa Ofisi ya makao makuu ya Wakala katika eneo la Maruhubi. Ambapo kwa sasa Mkandarasi ameshakamilisha hatua ya kusimamisha jengo na kumwaga zege katika ghorofa ya kwanza. Ni matarajio yetu kwamba katika robo ya kwanza ya 2021/22, ujenzi wa Ofisi ya Wakala utakuwa umekamilika.

**Programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali**

**76. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali ilipangiwa jumla ya

**shilingi bilioni 9.17** kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia Machi 2021, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya **shilingi milioni 25.16** kwa kazi za kawaida na maendeleo, sawa na **asilimia 0.3** ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa program ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali ulikuwa kama ifuatavyo:-

**Kutoa msaada kwa Wajasiriamali**

**77. Mheshimiwa Spika,** Jumla ya vikundi 57 vya Wajasiriamali vimetembelewa na kupewa ushauri wa Kitaalamu kwa viwanda vidogo vidogo na kati. Miongoni mwa vikundi hivyo ni; Kikundi cha ukamuaji mafuta ya alizeti Mafungwa na mradi wa ukamuaji wa mafuta ya nazi Vilima vinne Konde Pemba. Vikundi hivyo vilipatiwa utaalamu pamoja na fedha za kununulia malighafi ili kuimarisha utendaji kazi wao. Jumla ya TZS 5,500,000 zilitumika katika usaidizi huo.

**78. Mheshimiwa Spika,** Katika kuwaendeleza wajasiriamali, Wizara imefanya kikao kimoja (1) cha Kamati ya ushauri ya wajasiriamali ambayo inaundwa na wajumbe kutoka sekta ya umma na sekta binafsi. Kupitia vikao hivyo wajumbe walijadili juu ya kazi za wajasiriamali na mafanikio yao, changamoto wanazokumbana nazo pamoja na kutoa ushauri kwa Serikali juu ya namna bora ya kuendeleza sekta ya ujasiriamali. Pamoja

na hayo, imeonekana kwamba kuna mwamko mkubwa wa wananchi hasa vijana kujiajiri katika shughuli za ujasiriamali hasa kilimo na uzalishaji bidhaa.-

## PROGRAMU KUU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA BIASHARA

**79.** **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara inajumuisha Programu ndogo nne (4) ambazo ni Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji, Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji, Urahisishaji wa Biashara na Ukuzaji Biashara za Ndani pamoja na Usajili wa Biashara na Mali. Program hii ilipangiwa matumizi ya **shilingi bilioni 3.32** kwa mwaka wa fedha 2020 /2021. Hadi kufikia Machi 2021, programu hii imeingiziwa jumla ya **shilingi bilioni 1.268** ikiwemo Mishahara, Ruzuku, Miradi na kazi nyengine za uendeshaji, sawa na **asilimia 45** ya fedha zilizopangwa kwa kipindi kwa robo tatu. Fedha hizi ni sawa na asilimia **36** ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa kazi zilizopangwa katika kila program ndogo nilizozitaja ni kama ifuatavyo:

### Programu ndogo ya Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji

**80.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji inasimamiwa na Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko. Huduma ambazo

zimesimamiwa na kutekelezwa na Programu hii ndogo ni uimarishaji wa mazingira mazuri ya biashara pamoja na kuongeza Fursa za Masoko na Urahisishaji Biashara.

Program hii ndogo ilipangiwa jumla ya **shilingi milioni 856.30** kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia Machi 2021, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya **shilingi milioni 356.59** kwa ajili ya mishahara, kazi za maendeleo na kazi nyengine za kawaida sawa na asilimia **42** ya makadirio ya mwaka. Utekelezaji wa huduma za program ndogo hii ni kama ifuatavyo;

**Fursa za Masoko na Urahisishaji Biashara**

**81. Mheshimiwa Spika,** Wizara iliendelea kuangalia mwenendo wa masoko kwa bidhaa zetu pamoja na kuangalia changamoto zilizopo. Shughuli hii ilikwenda sambamba na jitihada ya Wizara kuzitangaza bidhaa zetu katika masoko ya Kanda ikiwemo ya Afrika Mashariki, SADC na AU.

**82. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Zanzibar katika maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba) yaliyofanyika Dar es Salaam mwezi wa Julai 2020. Taasisi sita (6) za Serikali zilishiriki katika maonesho hayo ambazo ni Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC), Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS), Shirika la

Bima la Zanzibar (ZIC), Kamisheni ya Utalii (ZCT), Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi ya Zanzibar (ZIPA) na Chuo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni pamoja na wajasiriamali 33 kutoka Unguja na Pemba. Bidhaa ambazo zilionyeshwa na Wajasiriamali walioshiriki katika maonesho hayo ni pamoja na bidhaa za kusindika, kazi za mikono, sabuni, dawa za asili, bidhaa za viungo (spices), mafuta ya mimea na nyenginezo. Aidha, Maonesho ya Sabasaba yaliweza kutoa fursa kwa wajasiriamali wetu kutangaza bidhaa zao na kuweza kupata wateja wengi zaidi. Kati ya wajasiriamali hao 5 wamepata soko (order) ya kuuza bidhaa zao baada ya maonesho kwa wateja mbali mbali. Kwa upande mwengine mauzo yaliyofanyika kwa wajasiriamali hao ni zaidi ya shilingi milioni 40.

83. **Mheshimiwa Spika,** Wizara katika hatua ya kuimarisha Mashirikiano ya kibiashara ya Kikanda na Kimataifa imeweza kushiriki katika mikutano mbali mbali ya Kikanda na Kimataifa yanayohusiana na maswala ya Biashara. Mikutano hiyo ni pamoja na vikao vya majadiliano ya uanzishwaji wa eneo huru la biashara barani Afrika (Continental Free Trade Africa), vikao vya itifaki ya biashara ya huduma Afrika Mashariki, mkutano wa kuwasilisha Sera ya Biashara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, vikao vya kuondosha vikwazo visivyo vya kiushuru (NTBs), vikao vya

urahisishaji biashara (Trade Facilitation), vikao vya usimamiaji wa maswala ya TBT na SPS, vikao vya SADC kwa lengo la kurahisisha ufanyaji biashara katika soko la Kikanda na Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** Katika eneo la Uanzishwaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Afrika uridhiaji huo umefikia takwa la kisheria la kutekeleza na kufanya kazi kwa mkataba huo, na ufunguaji wa biashara (tariff dismantling) umeanza rasmi tarehe 1 Januari 2021. Mkataba huo unatoa fursa ya kuwa na soko la pamoja lenye nchi 55 zenye takriban watu bilioni 1.2, Pato la Taifa la jumla ya zaidi ya Dola za Kimarekani trilioni 3.4 na fursa za uchumi unaokua kwa kasi. Vile vile, makubaliano ya mkataba huo yanatarajiwa kuongeza mchango wa Afrika kwenye soko la dunia kwa asilimia 2.8 huku sekta za kilimo, chakula na huduma zikipewa nafasi kubwa katika ukuaji huo. Hivyo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ipo katika hatua ya kwenda kuridhia Mkataba huo na kabla ya kwenda kurishidhia ilifanya kazi ya kupokea maoni ya michango ya wadau. Aidha kwa sasa Wizara inaendelea na hatua ya kupata maoni kutoka Serikalini.

84. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha kuwa wafanyabiashara na wajasiriamali wanaweza kupata masoko ya uhakika ya bidhaa zao, Wizara yangu iliratibu na kusimamia Tamasha la Saba

la Biashara lililofanyika kuanzia tarehe 4 hadi 17 Januari 2021, katika viwanja vya Maisara Zanzibar. Tamasha hilo lilifunguliwa rasmi tarehe 6 Januari, 2021 na Mhe. Samia Suluhu Hassan, (aliekuwa - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania). Kauli mbiu ya Tamasha la Saba la Biashara ilikuwa ni "Uchumi wa Buluu Kwa Maendeleo ya Biashara na Viwanda".

**85. Mheshimiwa Spika,** Jumla ya washiriki 328 walishiriki katika Tamasha la saba la biashara, kati yao taasisi za serikali ni 56, kampuni kubwa 31 na wafanyabiashara 241. Miongoni mwa wafanyabiashara hao washiriki watatu wanatoka nje ya nchi (Misri, Kenya na Burundi). Tamasha hili kama ilivyo kwa matamasha yaliotangulia limetowa fursa kwa wafanyabiashara, makampuni pamoja na Taasisi za umma na binafsi za ndani na nje ya nchi kuweza kunadi, kuzindua, kuonesha, kuuza bidhaa au huduma wanazozitoa. Pia limetowa fursa kwa wananchi kupata bidhaa tofauti zinazozalishwa ndani na nje ya nchi kwa bei nafuu. Makadirio ya mauzo yaliyofanyika katika Tamasha la Saba ni shilingi 1,276,368,364**/.**Vile vile, katika Tamasha la Saba kulikuwa na siku maalum (Special days) zenye maudhui mbalimbali, zikiwemo Siku maalum ya Ubunifu (ili kuibua vipaji vya vijana na wajasiriamali wengine) nayo ni ubunifu wa mashine na ubunifu wa technolojia ya habari na

mawasiliano (ICT) na Siku maalum ya uchumi wa buluu ili kujadiliana kuhusu ushiriki wa biashara na viwanda katika uendelezaji wa uchumi wa buluu. Kupitia kongamano la uchumi wa buluu wajumbe mbali mbali walichangia mada hiyo kwa lengo la kuzifikia na kuzitumia fursa zinazopatikana katika uchumi wa buluu.

86. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha kuwa uendeshaji wa biashara hauendi kinyume na sheria za usimamizi wa biashara nchini, Wizara imefanya ukaguzi katika maeneo ya wafanyabiashara ambao wameajiri wafanyakazi wa kigeni. Aidha jumla ya maombi 68 ya wafanyakazi wa kigeni yameshughulikiwa ya kuwaombewa ruhusa za kupata vibali vipya na wengine kuongezewa muda wa kufanya kazi na kuishi nchini.

87. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Mipango pamoja na MKURABITA imetoa mafunzo kwa wajasiriamali 50 walioko katika Wilaya ya Chakechake Pemba. Mafunzo hayo yamewalenga wajasiriamali kupata uwelewa kuhusiana na umuhimu wa kusajili biashara zao ili kuweza kutambulika kisheria na kuweza kupata fursa zinazopatikana katika kuendesha biashara katika mfumo rasmi. Aidha Wizara imeanzisha kituo Jumuishi cha urasimishaji biashara (One stop Center) katika Wilaya ya Mjini kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma za usajili

na leseni katika sehemu moja. Kituo hicho kimewaweka pamoja taasisi zilizofungamana moja kwa moja na biashara ambazo ni Manispaa ya mjini, ZFDA, BPRA, Mkemia Mkuu wa Serikali na ZRB. Kwa mfano, kituo jumuishi kimewezesha kuongezeka utowaji wa vibali kwa Mkemia mkuu wa Serikali hadi wastani wa vibali 10 kwa siku.

### Programu ndogo ya Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji

**88.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji inasimamiwa na Kitengo cha Mizani na Vipimo hapo awali na kwa sasa ni Wakala wa Vipimo, Zanzibar na Tume ya Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji. Program ndogo hii ilipangiwa jumla ya **shilingi milioni 376.87** kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia Machi 2021, programu hii imeingiziwa jumla ya **shilingi milioni 131.21** kwa ajili ya mishahara na kazi nyengine za kawaida sawa na asilimia **35** ya makadirio ya mwaka.

### Uimarishaji Ushindani Halali wa Kibiashara

**89.** **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji (ZFCC) ina jukumu la kusimamia masuala ya ushindani halali wa biashara baina ya wafanyabiashara na Makampuni, kuzuia mienendo ya biashara isiyo

ya ushindani pamoja na kudhibiti bidhaa bandia katika soko. Sambamba na kuzuia mienendo ya biashara isiofaa kama vile matumizi mabaya ya nguvu za soko, kushusha bei ili kumuondosha mshindani katika soko. Pia ina jukumu la kuhakikisha kila muekezaji, mwenye kiwanda, Mfanyabiashara na Mjasiriamali anafanya shughuli zake bila ya kumkwaza mwengine kwa ajili ya ustawi wa uchumi wa Zanzibar.

90. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Tume ya Ushindani Halali wa Kibiashara ilipangiwa jumla ya **shilingi milioni 155.80**. Hadi kufikia Machi 2021, Tume ya Ushindani imeingiziwa jumla ya **shilingi milioni 33.43** kwa ajili ya kazi nyengine za kawaida sawa na asilimia **21** ya makadirio ya mwaka.

91. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha ushindani halali wa kibiashara katika maeneo ya biashara, Wizara imefanya ukaguzi wa maduka 1,390 kati ya maduka 2,500 sawa na asilimia 56 ya ukaguzi huo, na kufanikiwa kukamata bidhaa zisizofaa kwa matumizi zenye jumla ya thamani ya shilingi 90,598,000. Bidhaa hizo ni kuku na samaki boksi 95 zenye thamani ya shilingi 4,800,000, Mchele paketi 232 wenye thamani ya shilingi 8,120,000 Tende paketi 26 yenye thamani ya shilingi 18,400,000, Taula za Watoto katuni 14 zenye thamani ya shilingi 1,134,000, Hamira

(Pasha) katuni 1,900 yenye thamani ya shilingi 55,423,000**,** losheni ya brand (rinju na rubi) boksi 21 zenye thamani ya shilingi 2,016,000 na bidhaa za makopo zenye thamani ya shilingi 705,000 bidhaa hizo ziliangamizwa kwa mujibu wa Sheria ya Ushindani wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji namba 5 ya mwaka 2018.

**92. Mheshimiwa Spika,** Kwa kuhakikisha tunamlinda Mtumiaji katika kupata huduma kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara kupitia Tume ya Ushindani Halali imekagua Mikataba ya Taasisi za kifedha kwa lengo la kupitia na kufanyia marekebisho ya masharti kandamizi kwa watumiaji. Aidha, Wizara imekamilisha kusahihisha Mikataba 66 iliyobainika ina masharti kandamizi.

**93. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Tume imehakikisha ufanisi wa kazi unapatikana kwa kufanya ununuzi wa vifaa vya kutendea kazi vikiwemo mafuta, vifaa vya kuandikia, Kompyuta mpakato pamoja na kulipia huduma za uendeshaji kama vile intaneti, umeme, gharama za posta na simu, huduma ya matangazo na matengenezo ya gari.

**94. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Vipimo Zanzibar imeundwa kwa Sheria Namba 6 ya mwaka 2020 (Zanzibar Weight and Measure Act

No. 6 of 2020) yenye lengo la kuweza kutoa huduma ya ulinganishi, pamoja na elimu juu ya aina na matumizi sahihi ya vipimo. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wakala wa Vipimo ilipangiwa jumla ya **shilingi milioni 209.6** katika kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia Machi 2021, Wakala wa Vipimo imeingiziwa jumla ya **shilingi milioni 61.38** kwa ajili ya ruzuku ya kazi za kawaida sawa na asilimia **29** ya makadirio ya mwaka.

**95.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Wakala ina jukumu la kufanya ukaguzi wa vipimo mbalimbali vikiwemo mizani, pampu za mafuta vituoni, mita za Bohari (Deport) pamoja na matangi ya kuhifadhia mafuta, Magari ya kusambazia mafuta na bidhaa zilizofungashwa. Idadi ya huduma za ukaguzi zilizofanywa kwa kipindi cha mwaka 2020/2021 ni kama zinavyoonekana katika **kiambatanisho namba 6.**

**96.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha ufanisi wa kiutendaji Wizara kupitia Wakala imefanya uzinduzi wa bodi ya Ushauri ya Wakala wa Vipimo pamoja na ununuzi wa vifaa vya Ofisi ikiwemo Meza 1, Viti 3, Kabati 1, Kompyuta 1 na Printa 1. Aidha, vipindi 3 vya kushajihisha elimu juu ya matumizi sahihi ya vipimo vimetolewa kwa njia ya redio na 1 kwa njia ya Televisheni.

### Programu ndogo ya Urahisishaji Biashara na Ukuzaji Biashara za Ndani

**97.** **Mheshimiwa Spika,** Program ndogo ya Urahisishaji Biashara na Ukuzaji Biashara za Ndani ilitekelezwa na Baraza la kusimamia mfumo wa Utoaji Leseni na Baraza la Taifa la Biashara ambapo ilipangiwa kutumia jumla ya **shilingi bilioni 1.22** kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia Machi 2021, programu hii ndogo imeingiziwa jumla ya **shilingi milioni 427.22** kwa ajili matumizi ya kazi za kawaida (Ruzuku) na kazi za maendeleo sawa na asilimia **35** ya makadirio ya mwaka. Programu ndogo ya Urahisishaji Biashara na Ukuzaji Biashara za Ndani ina jukumu la kutekeleza huduma zifuatazo:-

### Usimamizi wa Mamlaka zinazotoa Leseni

**98.** **Mheshimiwa Spika,** huduma hii ilitekelezwa na Baraza la Kusimamia Mfumo wa Utoaji Leseni ambalo lilipangiwa matumizi ya jumla ya **shilingi milioni 745.9** kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo shilingi milioni 345.9 kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi milioni 400.0 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2021, Baraza liliingiziwa jumla ya **shilingi milioni 279.95** kwa matumizi ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo sawa na asilimia **38** ya makadirio ya mwaka.

99. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Baraza lilifanya Mapitio ya leseni na ada kwa **Sekta ya kilimo** ambapo imezingatia uagiziaji na usafirishaji wa chakula, usafirishaji wa mazao ya mimea, miti na ukaguzi wa bidhaa. **Sekta ya Mifugo** imejumuisha usafirishaji na uingizaji wa wanyama na mazao ya mifugo ada za karantini, uhaulishaji wa wanyama, uchunguzi na matibabu ya wanyama. Kwa upande wa **Sekta ya uvuvi**, mapitio yamejumuisha ada za usajili na leseni za vyombo vya wavuvi wadogo wadogo, uvuvi wa kawaida na michezo ya Baharini na **Sekta ya maliasili na misitu** imejumuisha uhamishaji maliasili za misitu, fidia au uuzaji wa miti, bidhaa za misitu na miche katika vitalu vya Serikali. Kazi hii ya mapitio kwa sekta hizi itakamilika kwa kushirikiana na Mamlaka zinazosimamia sekta hizo. Mapitio kwa **sekta ya Biashara** yanajumuisha usajili wa Mkataba wa utoaji wa huduma na bidhaa kwa mtumiaji, ushindani wa kibiashara, ada za uhakiki wa Mizani na Vipimo, usajili wa biashara, mali bunifu, ubunifu wa viwanda, alama ya biashara na aina ya uasili wa kigeografia pamoja na vibali na ada za usimamizi wa viwango vya ubora kwa bidhaa zinazoingia na zinazozalishwa nchini.

100. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya ada **177** kwa sekta ya biashara zimefanyiwa mapitio kwa kuwekwa utaratibu mzuri wa utozaji kwa mfanyabiashara

kulipia leseni au kibali kwa huduma mara moja na kuunganisha ada za fomu ya maombi, usajili, matangazo na ukaguzi pamoja na kuunganisha ada za mizani ili kuondosha utitiri. Mapitio haya pia yamepelekea kupunguzwa baadhi ya ada ikiwemo vipimo kwa bidhaa zilizofungashwa ambapo viwanda vikubwa vitalipia shilingi 300,000 na vidogo vidogo kulipia shilingi 50,000 badala ya kufanya malipo kwa kila bidhaa. Ni matumaini yangu kwamba, hatua hii ya mapitio itapelekea kuweka utaratibu mzuri wa utozaji wa vibali, leseni na tozo hizo pamoja na kuondosha usumbufu kwa wafanyabiashara lakini pia hatua hii itaimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**101. Mheshimiwa Spika,** Baraza limekamilisha rasimu ya Mfumo wa utoaji wa leseni na ina mihimili miwili ambayo ni uwekaji taarifa za utoaji leseni na usimamizi wa utoaji leseni. Taarifa za Mamlaka zinazohusiana na sheria, aina ya leseni, mahitaji, ada, muda wa utoaji leseni, benki inayotumika na taarifa nyengine zimeshawekwa katika rasimu ya mfumo. Aidha mfumo umeandaa fomu itakayotumika na wafanyabiashara kwa ajili ya maombi ya leseni na Mafunzo ya usimamizi na utumiaji wa mfumo kwa maafisa wa leseni na Tehama yametolewa.

**102. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Baraza limefanya ukaguzi kwa

Mamlaka 31 za Utoaji leseni ikiwemo ZMA, ZFDA, ZBS, CGCLA, ZFCC, ZSHIPCO, ZPC, ZURA, WEMA, ZRB, LGAs, ZAWEMA, DTM, ZPRA, TRA, ZCRB, ZUMC na nyenginezo. Lengo ni kuangalia suala zima la kuondoa urasimu kwa kupunguza hatua, taratibu na muda wa upatikanaji leseni, vibali na ruhusa nyengine za ufanyaji biashara.

**Uimarishaji wa Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Serikali**

**103. Mheshimiwa Spika,** Serikali inatambua nafasi ya Sekta Binafsi kama injini ya maendeleo kwa Uchumi wa nchi. Kujenga Sekta Binafsi hasa kwa kutumia majukwaa ya majadiliano katika ngazi ya Taifa na ile ya Mikoa kutaiwezesha kuwawekea mazingira mazuri na rafiki. Majadiliano hayo yanalenga kuwasaidia wafanyabiashara kupata uwezo wa kupata mitaji, teknolojia rahisi na rafiki, masoko ya uhakika na huduma muhimu zinazolenga kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji ni suala lisilohitaji mijadala. Hivyo Serikali imeunda Baraza la Taifa la Biashara ambalo ni jukwaa maalum la majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na lengo kubwa ni kukabiliana na changamoto zinazoikabili sekta kuu za uchumi.

**104. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo yake, Baraza la Biashara la Taifa kwa mwaka wa

fedha 2020/21 lilipangiwa matumizi ya jumla za **shilingi milioni 470.0** ikiwa ni Ruzuku kwa ajili ya matumizi yake ya kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2021 Baraza la Taifa la Biashara liliingiziwa jumla ya **shilingi milioni 132.83** ikiwa ni sawa na asilimia 28 ya makadirio ya matumizi ya mwaka. Kazi zilizofanyika ni pamoja na:

i. Kuandaa Mikutano miwili ya Baraza la Taifa la Biashara pamoja na Majukwaa mawili (10 na 11) ya Baraza la Taifa la Biashara;

ii. Mikutano kumi ya Mabaraza ya Biashara ya Mikoa;

iii. Kufuatilia maazimio ya Jukwaa la Biashara pamoja na kuandaa taarifa za utekelezaji wa maazimio hayo; na

iv. Kufanya semina elekezi juu ya uelewa wa Baraza na Sheria yake kwa wadau pamoja mabaraza ya Mikoa.

105. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kulihakikishia Baraza lako kwamba Serikali itaendelea kuijenga Sekta binafsi ili iwe imara na ifikie lengo lake la kuwa injini ya Kukuza Uchumi na kuweza kufanya majadiliano endelevu baina yake na Sekta ya Umma.

### Programu ndogo ya Usimamizi wa Usajili wa Biashara na Mali

**106. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Usimamizi wa Usajili Biashara na Mali ilitekelezwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA) ambayo ilipangiwa matumizi ya jumla ya **shilingi milioni 867.70** kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 na hadi kufikia Machi 2021, Wakala iliingiziwa jumla ya **shilingi milioni 338.14** kwa matumizi ya ruzuku ya kazi za kawaida sawa na asilimia **39** ya makadirio ya mwaka.

**107. Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la kuanzishwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (BPRA) kufanya usajili wa biashara na mali ikijumuisha hati za mali ubunifu pamoja na usajili wa nyaraka mbalimbali zinazowahusu wananchi na wageni wanaofanya shughuli zao Zanzibar. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2020/2021 BPRA imeweza kusajili Kampuni 755, Majina ya Biashara 889, Alama za biashara 199 na Nyaraka 1,001.

**108. Mheshimiwa Spika,** Katika kuelimisha jamii juu ya ufahamu wa usajili wa biashara na mali, BPRA imefanya vipindi mbalimbali pamoja na kutoa matangazo ya kuhamasisha kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) na kituo cha habari cha Bomba FM. Pia imefanya mkutano wa wadau

kuhusu usajili wa marudio kwa taasisi za biashara ambazo zilishindwa kufanya usajili wa marudio kwa taasisi zilizosajiliwa kabla ya kuanza kutumika mfumo. Aidha, BPRA imeshiriki katika Tamasha la 7 la Maonesho ya Biashara lililofanyika katika viwanja vya Maisara.

109. **Mheshimiwa Spika,** Katika utoaji mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu BPRA imewapatia mafunzo ya muda mfupi Wafanyakazi 3. Mafunzo hayo ni ya'International Standard Industrial Code' ISIC yaliyofanyika Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar. Pia Ofisi imefanya mafunzo ya ndani ya usimamizi mfumo wa usajili wa biashara kwa kushirikiana na Mtaalamu wa ndani kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).

## PROGRAMU KUU YA VIWANGO NA TATHMINI YA UBORA

110. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Viwango na Tathmini ya Ubora inasimamiwa na Taasisi ya Viwango Zanzibar, inajumuisha Programu moja ndogo ambayo ni Viwango na Uthibiti wa Ubora. Programu hii ilipangiwa matumizi ya **shilingi bilioni 3.94** kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia Machi 2021, programu hii imeingiziwa jumla ya **shilingi bilioni 668.38** ambayo ni Ruzuku ya mishahara ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo sawa na asilimia **17** ya makadirio

ya mwaka. Utekelezaji wa huduma zilizopangwa katika program ndogo niliyoitaja hapo juu ni kama ifuatavyo:

**Programu ndogo ya Viwango na Udhibiti wa Ubora**

**Uandaaji na Ukuzaji wa Viwango**

**111. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Viwango imeendelea na jukumu lake la kuandaa viwango ambapo jumla ya viwango vipya 141 vimeandaliwa na kuidhinisha sawa na asilimia 176 ya lengo la uandaaji viwango. Kati ya hivyo viwango 45 vya Chakula, 17 uhandisi mitambo na vyombo vya moto, 52 kemikali, 26 mazingira na 1 Utalii. Aidha, jumla ya sampuli 795 zimefanyiwa uchunguzi wa kimaabara sawa na asilimia 96 ya lengo kwa mwaka. Matokeo ya ripoti hizo za uchunguzi wa kimaabara kwa bidhaa za kawaida yanaonesha kwamba sampuli za bidhaa 741 zimekidhi vigezo vya viwango husika na sampuli 54 zimebainika kutokukidhi viwango husika.

**112. Mheshimiwa Spika,** Katika kusimamia viwango wa bidhaa, Taasisi ya viwango imetoa leseni za alama ya ubora 6 sawa na asilimia 38 ya lengo kwa mwaka. Bidhaa zilizopatiwa leseni ya alama ya ubora ni pamoja na Korosho, Chaki za kuandikia shuleni, "Re-usable Pads", Mafuta ya

mgando ya pendeza, Maji ya kunywa ya “Super Pure” na Maji ya kunywa ya “Drop of Zanzibar”.

## Uthibiti wa Ubora wa Bidhaa

113. **Mheshimiwa Spika,** Uthibiti Ubora wa bidhaa unaendelea kufanyika kwa bidhaa zinazoingia na kuzalishwa nchini. Wizara kupitia Taasisi ya Viwango imefanya ukaguzi wa bidhaa na imefanikiwa kutoa Vyeti vya ubora wa bidhaa nyenginezo (General goods) 533 kwa kutumia mfumo wa ukaguzi wa nje ya nchi (PVoC). Shehena za bidhaa 3,113 na gari 2,985 zimekaguliwa kupitia mfumo wa ukaguzi wa ndani ya nchi (DI). Shehena 91 za mafuta ya nishati zimekaguliwa kati ya hizo shehena 33 za Dizeli, 39 za Petrol, 11 mafuta ya taa na 8 mafuta ya ndege (Jet A1).

114. **Mheshimiwa Spika,** Katika mradi wa kuimarisha Taasisi viwango unaohusiana na ujenzi wa Ofisi na Maabara na Ununuzi wa vifaa vya Maabara ujenzi umefikia asilimia 65. Aidha, ujenzi wa ukuta wa eneo la kukagulia vyombo vya moto Mwembemakumbi umekamilika.

## SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC):

115. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Shirika liliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango Mkakati

wa Shirika (Corporate Strategic Plan) ya miaka mitano 2021-2025. Katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Shirika lilikabiliwa na msimu mdogo wa vuno la Karafuu na kushuka kwa bei ya karafuu katika soko la dunia ambao umepelekea kuwepo kwa changamoto katika utekelezaji wa majukumu yake. Hata hivyo, Shirika liliendelea kuimarisha bidhaa linazozalisha, kuimarisha majengo kwa lengo la kuongeza kipato na kuhuisha ustawi wa Shirika kwa kuhakikisha kwamba mashirikiano na wadau wa zao la karafuu na bidhaa nyengine yanaimarishwa.

116. **Mheshimiwa Spika**, Shirika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiria kukusanya jumla ya **shilingi bilioni 45.7** kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato vikiwemo; Mauzo ya karafuu na mafuta ya mimea, mapato yanayotokana na majengo na mapato mengineyo. Hadi kufikia Machi,2021 Shirika limeweza kukusanya jumla ya **shilingi bilioni 5.4** ambazo ni sawa na asilimia 12 ya makadirio ya mwaka mzima. Hii imetokana na msimu kuwa mdogo sana kinyume na matarajio na hivyo upatikanaji wa karafuu kuwa mdogo.

117. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi Shirika lilipanga kutumia jumla ya **shilingi bilioni 73.67** ikiwa ni matumizi ya kawaida ya gharama za uendeshaji, ununuzi wa karafuu

na maendeleo, ambapo hadi kufikia machi 31, Shirika limefanikiwa kutumia jumla ya **shilingi bilioni 7.53** sawa ya asilimia **10** ya makadirio kwa mwaka.

118. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Shirika lilijipangia kununua **tani 3,500** za karafuu kavu kwa gharama ya **shilingi bilioni 40.2** hadi kufikia machi, 2021 shirika limeweza kununua tani 213 za karafuu kavu kutoka kwa Wakulima kwa gharama ya **shilingi bilioni 2.9**. Karafuu zilizonunuliwa ni sawa na asilimia 6 ya makadirio kwa mwaka. Kupungua kwa manunuzi ya karafuu kwa mwaka 2020/2021 kumesababishwa na kuwepo kwa msimu mdogo wa karafuu. Pia, Shirika limefanya manunuzi ya Makonyo **tani 23.82** zenye thamani ya **shilingi milioni 35.73**. Pamoja na kufanya ukarabati mdogo wa Kiwanda cha Makonyo.

## 5 CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2020/2021:

119. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio makubwa katika utekelezaji wa malengo na majukumu mbali mbali ya Wizara kwa mwaka 2020 /2021, pia zipo changamoto zilizoathiri utekelezaji wa malengo yaliyopangwa katika sekta ya biashara na viwanda. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

i. Mripuko wa gonjwa la Corona ambao kwa kiasi kikubwa umeathiri sekta za Utalii, fedha, Mawasiliano, usafirishaji, Biashara na Uwekezaji ambao ndio wadau wetu wakubwa katika kufikia malengo

ii. Kutotumika kwa mfumo wa Usajili wa Mikataba ya Amana kwa Mali zinazohamishika. Pamoja na jitihada kubwa zilizochukuliwa na BPRA za kuitangaza na kuelimisha jamii na taasisi za fedha (Bank) kwa njia mbalimbali juu ya uwepo wa Sheria ya Mikataba ya Amana kwa Mali zinazohamishika Nam, 4 ya mwaka 2011 bado taasisi hizo za fedha hazijawa tayari kutoa mikopo chini ya Sheria hiyo kwa wajasiriamali.

iii. Kushuka kwa bei ya Karafuu katika soko la Dunia kumeathiri kwa kiwango kikubwa shirika letu za ZSTC, ikiwa ni pamoja na kukosa kulipa mikopo na kuendesha taasis.

iv. Kuendelea kuwepo kwa vikwazo vya kibiashara ambavyo ni vya kiushuru (VAT, import duty) na visivyo vya kiushuru (NTB) kati ya Tanzania Bara na Zanzibar. Kwa mfano, wazalishaji wadogo ambao wanazalisha bidhaa zenye uasili wa Zanzibar (sabuni) wanatozwa ushuru wa forodha

(importy duty) wa asilimia 25 kama vile bidhaa hio imeingizwa kutoka nje ya nchi.

v. Mazingira mazuri ya Ofisi ya kufanyia kazi, ni moja ya Changamoto kubwa. Wizara ipo katika majengo ya zamani ya mji Mkongwe ambayo hayana haiba nzuri na nafasi ya kutosha kwa Wafanyakazi wote wa Wizara, hali iliyopelekea Idara za Wizara kuwa katika majengo tofauti tofauti.

## 6 PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA 2021/2022:

**120. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda katika utekelezaji wa majukumu yake imepanga vipaumbele vyake kwa kuzingatia kasi ya Serikali ya awamu ya nane ya kuendeleza viwanda kama ilivyoelezwa katika Ilani ya CCM ya mwaka 2021-2025, Dira ya Zanzibar 2050, Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA III 2016-2020), Mpango Kazi wa Ahadi za Mheshimiwa Rais, 2021-2025 pamoja na miongozo ya Viongozi na Wakuu wa nchi yetu. Maeneo mengine makuu yatakaopewa kipaumbele ni pamoja na kuweka mazingira mazuri ya Biashara, kupanua wigo wa vipimo, utafutaji wa masoko na usaidizi wa wajasiriamali na wazalishaji wadogo wadogo.

121. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda inatarajia kutekeleza shughuli mahsusi zifuatazo katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2021/2022 kama vipaumbele vyake:-

i. **Kuyaendeleza Maeneo ya Viwanda:** Wizara inatarajia kuliendeleza Eneo la Viwanda la Dunga kwa kupima, kuandaa Mpango wa Matumizi ya ardhi, kufikisha miundombinu ya umeme, maji na kukata barabara za ndani. Kwa upande wa eneo la viwanda la Nungwi, Wizara inafanya tathmini ili kulipa fidia na kuandaa gharama za kuweka miundombinu.

ii. **Kuongeza udhibiti wa ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini na zinazozalishwa nchini kwa kuimarisha maabara za upimaji kwa kununua vifaa na Ujenzi wa Ofisi ya ZBS:** Wizara inatarajia kukamilisha ujenzi wa ofisi na Maabara eneo la Maruhubi. Wizara kupitia ZBS pia inatarajia kufanya ununuzi wa vifaa vya kisasa vya maabara ili kuimarisha mifumo ya udhibiti ubora wa bidhaa za ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara inatarajia Kuimarisha utekelezaji wa Mfumo wa Ubora ndani ya ZBS (QMS) kwa kutumia kiwango cha **ISO 9001:2015.**

iii. **Kuendeleza Uwanja wa Maonesho wa Kimataifa wa Zanzibar (Nyamanzi):**
Eneo la Nyamanzi limewekwa katika orodha ya Miradi ya kuendelezwa Kwa kushirikiana na sekta binafsi (PPP), hivyo kwa mwaka huu wa fedha, Wizara inakusudia kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira na kijamii (ESIA). Kwa upande mwingine, Wizara itaanza kwa hatua za awali kusafisha eneo, kupeleka miundo mbinu ya maji, umeme na barabara.

iv. **Kusimamia na kuratibu uwezeshaji wa matumizi ya Mfumo mpya wa utoaji leseni kwa njia ya kielektoniki kwa Mamlaka za utoaji leseni:**
Ili kuendelea kurahisisha ufanyaji biashara hapa Zanzibar, Wizara kupitia Baraza la Kusimamia Mfumo wa Utoaji Leseni (BLRC) itaratibu na kusimamia mfumo wa utoaji leseni kwa njia ya kielektroniki ambao utahusisha mamlaka zote za utoaji leseni hapa. Pamoja na kuendelea kufanya mapitio ya tozo mbalimbali.

v. **Kukamilisha Ujenzi wa Makao Makuu ya SMIDA:**
Wizara inatarajia kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya SMIDA iliyopo Maruhubi, ili kuhakikisha watendaji wa SMIDA wanapata mazingira mazuri ya kufanyia kazi pamoja na kutoa huduma kwa wazalishaji.

vi. **Kuwakuza na kuwaendeleza Wajasiriamali kwa kuwapatia mikopo:**
Kupitia Programu ndogo ya kuwaendeleza wajasiriamali, Wizara itatoa mafunzo na mikopo kwa wazalishaji wadogo wadogo kutoka Halmashauri na Miji ya Zanzibar na makundi maalum ya vijana na wanawake ili kuwapatia mitaji na kuweza kujiajiri.

vii. **Kujenga uwezo kwa Wajumbe wa Mabaraza ya Mikoa:**
Wizara inatarajia kufanya vikao mbali mbali vya kutoa uelewa kwa ngazi za Mikoa na Wilaya zote Unguja na Pemba, kwa kufanya hivi itasaidia kuwajengea uwezo na kuwaongezea maarifa ya utambuzi wa masuala mbalimbali yanayoweza kuleta tija nchini.

viii. **Kufanya tafiti za kuendeleza biashara na viwanda:**
Wizara inatarajia kufanya tafiti mbalimbali ikiwemo leseni na vibali vya biashara, usafirishaji na uingizaji wa bidhaa kutoka Tanzania bara, uzalishaji viwandani na utafiti wa kuainisha Masoko kwa bidhaa zinazozalishwa Zanzibar.

ix. **Kuimarisha Baraza la Ushindani Zanzibar**
Kwa sasa Baraza tayari limeanzishwa kwa mujibu wa sheria, hivyo Wizara inatarajia kuweka mikakati imara itakayopelekea Baraza

kusikiliza mashauri ya ushindani na kuyatolea maamuzi ili kuweka mazingira ya usawa na ushindani halali katika soko. Mikakati hiyo ni pamoja na kutayarisha kanuni ya kuendesha Baraza, kulitangaza Baraza kwa Wadau, Kuandaa muundo wa Baraza na kupata rasilimali watu.

x. **Kuanzisha na kuendeleza Sekta ya Tehama ya Viwanda**
Teknolojia ya Habari na mawasiliano (Tehama) ni nyezo muhimu ambayo mchango wake ni mkubwa katika kuharakisha kufikiwa kwa malengo ya uchumi wa Viwanda. Wizara inataanzisha na kuendeleza sekta ya Tehama ya Viwanda ili kuhakikisha wananchi wanapata taarifa kuhusu shughuli mbalimbali zitakazokuwa zinatekelezwa katika sekta hii.

xi. Kuendelea kuondosha Urasimu katika utoaji wa leseni kupitia Majadiliano ya sekta binafsi na mamlaka pamoja na kufanya mapitio ya taratibu, muda na hatua za utoaji leseni, vibali na ruhusa za ufanyaji biashara kisekta.

xii. Kukamilisha mfumo wa kitaifa wa utoaji leseni na kuunganisha Mamlaka za utoaji leseni ili kurahisisha upatikanaji wa leseni kwa wafanyabiashara. Hatua hii itajumuuisha kuendelea na uwekaji wa taarifa za mamlaka

na usimamizi wa mfumo, ununuzi wa vifaa, utoaji wa mafunzo kwa mamlaka na wafanyabiashara.

**xiii.** Kufanya mapitio ya sheria na kuandaa kanuni za mbalimbali zinazo kwamisha maendeleo ya biashara na viwanda pamoja na zile ambzo hazikidhi hali ya sasa.

**xiv.** Kufanya Ununuzi wa karafuu tani 7,000 na makonyo tani 1200. Vile vile Kuongeza uzalishaji katika mafuta ya mimea kwa kuimarisha mashamba yake pamoja na kukiimarisha zaidi Kiwanda cha mafuta ya Makonyo na Arki za mimea.

**xv.** Kuimarisha ukulima wa zao la mwani kwa kutafuta masoko yenye tija. Ambapo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Shirika linatarajia kununua jumla ya tani 1000 za mwani kwa gharama ya TZS 920.0 milioni. Pamoja na Kuratibu na kuanzisha Kiwanda cha kusarifu Mwani

**122.** **Mheshimiwa Spika** Kwa mwaka wa fedha 2021/22, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imepangiwa matumizi ya jumla ya **shilingi bilioni 30.545.** Kati ya fedha hizo Jumla ya **shilingi bilioni 9.67** zimetengwa kwa ajili ya Matumizi ya kazi za kawaida na Mishahara na

**shilingi bilioni 20.88** kwa kazi za Maendeleo. Fedha za maendeleo ni pamoja na **Shilingi bilioni 4.6** tunazotarajia kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa programu ya kuendeleza Viwanda.

**123. Mheshimwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2021/22 Wizara ya Biashara na Viwanda imepanga kutekeleza miradi 2 ya maendeleo ambayo ni: Mradi wa kuendeleza Viwanda na Mradi wa Kuimarisha Mazingira bora ya biashara iliojumuisha shughuli za kuanzisha na kuendeleza maeneo ya Viwanda, Ujenzi wa Ofisi na Maabara za ZBS, Kuimarisha eneo la Uwanja wa Maonesho wa Kibiashara, Kutoa mikopo na kuwajengea uwezo wajasiriamali.

**124. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara Biashara na Maendeleo ya Viwanda itatekeleza program kuu tatu (3) na program ndogo nane (8). Programu kuu hizo kama zifuatavyo:

i. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara

ii. Programu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali

iii. Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara

## PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA BIASHARA NA VIWANDA

125. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Viwanda imegawika katika Programu ndogo tatu kwa mujibu wa huduma ambazo inazitoa. Program hizo ndogo ni kama zifuatazo:

i. Utawala na Uendeshaji wa shughuli za Wizara ya Biashara na Viwanda;

ii. Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara; na

iii. Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba

126. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa shughuli za Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ambayo inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi itakuwa na jukumu la kutoa huduma ya usimamizi wa rasilimali watu na huduma za kiofisi kwa ujumla pamoja na ununuzi wa vifaa. Ili kutekeleza majukumu yake, program hii ndogo imepangiwa matumizi ya **shilingi bilioni 1.86** kwa mwaka wa fedha 2021/ 2022.

127. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa program ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za

Wizara ambayo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, itakuwa na jukumu la uandaaji na uibuaji wa sera na tafiti za Wizara, uandaaji na utekelezaji wa mipango ya Wizara pamoja na usimamizi wa takwimu za Biashara na Viwanda. Katika kutekeleza huduma hizo, programu ndogo ya uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti imepangiwa matumizi ya **shilingi milioni 576.13** kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022.

128. **Mheshimiwa Spika,** Program ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba ambayo inaratibu shughuli za uendeshaji wa Wizara ya Biashara na Viwanda kwa upande wa Pemba imepangiwa matumizi ya **shilingi milioni 602.85** kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022.

129. **Mheshimiwa Spika,** Ili kuweza kutekeleza shughuli zilizopangwa katika Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Viwanda kwa mwaka 2021 – 2022, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya **shilingi bilioni 3.04** kwa program hii kuu.

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI

130. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali imegawika

katika Programu ndogo mbili kwa mujibu wa huduma ambazo inazitoa. Program hizo ndogo ni kama zifuatazo:

i. Ukuzaji Viwanda

ii. Maendeleo ya Ujasiriamali

131. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Ukuzaji Viwanda itakuwa na jukumu la kutoa huduma ya Uimarishaji wa Sekta ya Viwanda, Uratibu na utekelezaji wa Sera ya MSME's na Ukuzaji wa MSME's na uendelezaji wa ujasiriamali utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda na SMIDA. Ili kutekeleza huduma hii, programu hii ndogo imepangiwa matumizi ya **shilingi bilioni 3.36** kwa mwaka 2021/2022.

132. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali ambayo ina jukumu la kutoa kuwakuza na kuwaendeleza wajasiriamali, Ili kutekeleza programu hii ndogo imetengewa **shilingi bilioni 10.36** kwa mwaka 2021/2022.

133. **Mheshimiwa Spika,** Ili kutekeleza majukumu ya Program kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali kwa mwaka 2021/2022, naomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya **shilingi bilioni 13.72** kwa ajili ya kutekeleza shughuli za programu hii kuu.

## PROGRAMU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI BIASHARA

134. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya tatu itakayotekelezwa na Wizara kwa mwaka 2021/2022 ni Ukuzaji na Uendelezaji Biashara. Kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa malengo yake, programu hii imegawanyika katika Programu ndogo tatu (3) kama zifuatavyo:

   i. Ukuzaji Masoko na Usafirishaji

   ii. Uwezeshaji Biashara

   iii. Utengamano wa Kibiashara

135. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Ukuzaji Masoko na Usafirishaji itakuwa na jukumu la kutoa huduma za uimarishaji wa mazingira mazuri ya biashara, kuongeza fursa za masoko kwa bidhaa za Zanzibar pamoja na urahisisishaji biashara ambapo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Biashara. Ili kutekeleza majukumu hayo, programu ndogo ya Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji imetengewa **shilingi bilioni 4.640** kwa mwaka 2021/2022.

136. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa programu ndogo ya Uwezeshaji Biashara itakuwa na jukumu la kuharakisha utoaji wa bidhaa na kuboresha taratibu za utoaji mizigo pamoja na kupunguza

taratibu, gharama na muda wa usafirishaji na uingizaji bidhaa nchini. Ambapo utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Biashara, Wakala wa Vipimo, Tume ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji, Baraza la Taifa la Biashara, Wakala wa Usajili Biashara na Mali, Baraza la Ushindani, Taasisi ya Viwango na Baraza la Mfumo wa Utoaji Leseni. Ili kutekeleza jukumu hili, naliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya **shilingi bilioni 9.036** kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**137. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utengamano wa Kibiashara wenye jukumu la kuimarisha biashara huria inayopelekea upanuzi wa sokona kuongeza biashara baina ya nchi na nchi utasimamiwa na Idara ya Biashara.Ili kutekeleza jukumu hili lililopangwa chini ya Programu hii ndogo, naliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya **shilingi milioni 108.090.**

**138. Mheshimiwa Spika,** Ili kutekeleza huduma zilizopangwa katika Programu kuu hii ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara kwa mwaka 2021/2022, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya **shilingi bilioni 13.785** kwa program hii kuu.

## SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA – ZSTC

Shughuli za Shirika kwa mwaka wa fedha 2021/2022

139. **Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/ 2022, Shirika la Biashara la Taifa linatarajia kutekeleza shughuli kuu zifuatazo;

i. Ununuzi wa karafuu tani 7,000 na makonyo tani 1,200;

ii. Kuongeza uzalishaji katika mafuta ya mimea kwa kuimarisha mashamba yake pamoja na kukiimarisha zaidi Kiwanda cha mafuta ya Makonyo na Arki za mimea.

iii. Kuimarisha kilimohai kwa kukiimarisha kituo maalum cha kilimohai katika eneo la Saateni pamoja na kuongeza wazalishaji.

iv. Kuimarisha ukulima wa zao la la mwani kwa kutafuta masoko yenye tija. Ambapo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Shirika linatarajia kununua jumla ya tani 1000 za mwani kwa gharama ya TZS 920.0 milioni.

### Ununuzi na Mauzo ya Karafuu

140. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, bei ya kununulia Karafuu kutoka kwa Mkulima ni asilimia 80 ya bei itakayokuwepo Sokoni. Bei ya kununulia mwani kwa kilo kwa mwani aina ya Cottonii ni TZS 1,800 na TZS 700

kwa kilo kwa mwani aina ya Spinosum. Makonyo yatanunuliwa kutoka kwa mkulima kwa bei ya TZS 1,500.00 kwa kilo.

**140. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021 /2022, Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Biashara la Taifa limeidhinisha matumizi ya Jumla ya **shilingi bilioni 84.1** katika kutekeleza kazi za kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 61.5 ni kwa ajili ya ununzi wa Makonyo na Karafuu.

## 7 SHUKRANI:

**141. Mheshimiwa Spika,** mafanikio ya Wizara yaliyopatikana ni matokeo ya mashirikiano makubwa ya Wajumbe wa Baraza hili chini ya uongozi wako mahiri. Ninakushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati za kudumu za Baraza na Wajumbe wote kwa ushauri na michango mliyotupa katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti. Shukrani zangu pia ziende kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii Mheshimiwa Ali Suleiman (Mrembo), Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele, wajumbe na Makatibu wote wa Kamati hiyo kwa ushauri na miongozo waliyoitoa katika mapendekezo ya Bajeti ya Wizara na hatimae kuridhia mapendekezo haya yawasilishwe katika Baraza hili.

**142. Mheshimiwa Spika,** mafanikio ya kiutendaji yaliyojitokeza katika kipindi cha mwaka 2020/2021 ni matokeo ya ushirikiano mkubwa uliopatiwa Wizara yangu kutoka wadau mbali mbali wa ndani na nje ya nchi yetu. Kwa madhumuni ya kutambua mchango mkubwa wa Wadau hao kwa Wizara, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa nchi na taasisi za ndani na nje zifuatazo; Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO), Shirika la Kimataifa la Tasnia ya Malibunifu (WIPO), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), TradeMark East Africa (TMEA), Shirika la Biashara Duniani (WTO), TANTRADE, REPOA, Zanzibar Seaweed Cluster Initiative (Zasci), Jumuiya za Wafanyabiashara, Zanzibar (ZNCC) na Wafanyabiashara na Wawekezaji wa Viwanda wote wakubwa na wadogo.

**143. Mheshimiwa Spika,** napenda nichukue fursa hii kwa mara nyingine tena kuwapongeza kwa dhati wafanyakazi wote wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa kazi kubwa yenye ufanisi mzuri wanayoifanya kila siku licha ya kukabiliwa na changamoto mbali mbali, ni matarajio yangu kwamba wataongeza juhudi zao ili kuzidisha ufanisi kwa kuwahudumia wananchi na kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Kadhalika, napenda kuwapongeza wafanyakazi wote walioshiriki katika maandalizi ya Hotuba

hii kwa kazi nzuri waliyoifanya, nawaombea dua njema katika kazi zao.

# 8 MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022:

## 8.1 Mapato ya Serikali

**144. Mheshimiwa Spika, k**wa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara yangu imepanga kukusanya jumla ya **shilingi 2,835,626,000** Mapato hayo yatakusanywa kutoka vianzio vifuatavyo kama inavyoonekana katika **Jadweli Nam. 4:**-

## Jadweli Nam. 4:
## Mapato ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021 - 2022

| KIFUNGU | MAELEZO | MAKADIRIO |
|---|---|---|
| **R0113** | **Wakala wa Vipimo** | **137,002,000** |
| **1422014** | Ukaguzi wa Mezani na Vipimo | 137,002,000 |
| | | |
| **R0105** | **Idara ya Uendeshaji na Utumishi** | **236,242,000** |
| 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo ya Kibiashara | 236,242,000 |
| | | |
| **R0106** | **Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali** | **751,395,000** |
| **1146002** | Ada ya Utunzaji Urithi | 1,876,000 |
| **1422030** | Alama za Biashara | 360,109,000 |
| **1422031** | Uandikishaji wa Makampuni | 260,394,000 |
| **1422032** | Uandikishaji wa Majina ya Biashara | 77,503,000 |
| **1422034** | Ujira wa kutengeneza Nyaraka | 51,513,000 |
| | | |
| **R0107** | **Taasisi ya Viwango Zanzibar** | **1,054,059,000** |
| 1112008 | Malipo yatokanayo na Usimamizi wa Viwango | 1,054,059,000 |
| | | |
| **R0109** | **Tume ya Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji** | **583,028,000** |
| 1422077 | Malipo ya Kazi za Biashara | 583,028,000 |
| | | |
| **R0101** | **Ofisi Kuu Pemba** | **73,901,000** |
| **1422014** | Ukaguzi wa Mezani na Vipimo | 42,661,000 |
| **1422034** | Ujira wa Kutengeneza Nyaraka | 15,483,000 |
| **1422078** | Ukodishaji wa Maeneo Kibiashara | 15,757,000 |
| **Jumla Kuu** | | **2,835,626,000** |

***Chanzo: Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, 2021***

## 8.2 Matumizi

145. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi na ili Wizara yangu iweze kutekeleza programu zake ilizojiwekea kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya jumla ya **shilingi 30,544,500,000** kwa programu tatu (3) kama inavyoonekana katika **Jadweli Nam. 5**:

### Jadweli Nam. 5:
### Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2021/2022 (TZS Mil)

| KIFUNGU | Programu Kuu/ Programu Ndogo | Makadirio |
|---|---|---|
| **PR0101** | **Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda** | **3,037,903,000** |
| SR010101 | Utawala na Uendeshaji | 1,858,921,000 |
| SR010102 | Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara | 576,126,000 |
| SR010103 | Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba | 602,856,000 |
| | | |
| **PR0102** | **Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali** | **13,721,173,000** |
| SR010201 | Ukuzaji wa Viwanda | 3,356,988,000 |
| SR010202 | Maendeleo ya Ujasiriamali | 10,364,185,000 |
| | | |
| **PR0103** | **Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara** | **13,785,424,000** |
| SR010301 | Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji | 4,640,773,000 |
| SR010302 | Uwezeshaji wa Biashara | 9,036,561,000 |
| SR010303 | Utengamano wa Biashara | 108,090,000 |
| JUMLA KUU | | **30,544,500,000** |

***Chanzo: Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, 2021***

## 9 HITIMISHO:

146. **Mheshimiwa Spika,** naomba kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako na wananchi kwa ujumla kwa kunisikiliza.

147. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

# 10 VIAMBATANISHO:

## Kiambatanisho namba 1:

## Usafirishaji (Export) kwenda Nchi za SADC, 2016-2020

Thamani (Milioni)

| Nchi zaJumuiya ya SADC | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| Botswana | - | - | - | 4.6 | - |
| Congo (Kinshasa) | - | - | 9.2 | 2.5 | - |
| Congo (Brazzaville) | 0.1 | - | 4.6 | - | - |
| Comoros | 426.0 | 994.5 | 676.7 | 538.4 | 491.3 |
| Mauritius | - | - | - | - | - |
| Malawi | 4.6 | - | - | - | 158.9 |
| Mozambique | 128.4 | 23.3 | 10.7 | 7.6 | 17.6 |
| South Afrika | 63.3 | 350.9 | 200.2 | 121.7 | 18.8 |
| Zambia | 435.5 | 218.8 | 111.8 | 23.1 | 111.9 |
| Zimbabwe | - | - | - | 0.4 | - |
| **Jumla** | **1,057.9** | **1,587.5** | **1,013.2** | **698.3** | **799.2** |

*Chanzo: Annual External Mechandize Trade Statistics, 2021*

## Kiambatanisho namba2:

## Uagiziaji (Import) kutoka Nchi za SADC, 2016-2020

Thamani (Milioni)

| NchizaJumuiyaya SADC | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| Botswana | 10.2 | 0.4 | 0.9 | - | - |
| Congo (Kinshasa) | - | 6.1 | - | - | - |
| Congo (Brazavile) | 0.1 | - | 0.3 | - | - |
| Comoros | 11.4 | 16.9 | 26.6 | 7.8 | 14.5 |
| Lesotho | - | - | - | - | 0.1 |
| Madagascar | - | 24.7 | - | - | - |
| Mauritius | 196.5 | 518.9 | 615.7 | 3,477.1 | - |
| Malawi | 39.1 | - | - | 6.4 | 0.1 |
| Mozambique | 11.7 | - | 3,187.3 | - | 102.9 |
| Namibia | - | 2.2 | - | - | 0.2 |
| Seychelles | - | - | 2.3 | - | - |
| Swaziland | 45.1 | 394.9 | 1,872.1 | 11,447.7 | 210.1 |
| South Afrika | 3,717.7 | 2,391.4 | 7,572.0 | 8,896.0 | 5,830.2 |
| Zambia | - | 4.5 | 0.1 | - | - |
| Zimbabwe | 58.4 | 79.1 | 35.1 | - | - |
| **Jumla** | **4,090.2** | **3,439.1** | **13,312.4** | **23,827.0** | **6,158.1** |

*Chanzo: Annual External Mechandize Trade Statistics, 2021*

# Kiambatanisho namba 3:

## Mapato ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020 - 2021

| KIFUNGU | MAELEZO | Makadirio Julai 2020 –Juni 2021 | Makusanyo Julai 2020 –Machi, 2021 | Asilimia ya Makusanyo |
|---|---|---|---|---|
| **R0104** | **Wakala wa Vipimo** | **154,400,000** | **64,210,331** | **42** |
| **1422014** | Ukaguzi wa Mezani na Vipimo | 154,400,000 | 64,210,331 | 42 |
| | | | | |
| **R0105** | **Idara ya Uendeshaji na Utumishi** | **197,268,000** | **37,770,000** | **19** |
| 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo Kibiashara | 197,268,000 | 37,770,000 | 19 |
| | | | | |
| **R0106** | **Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali** | **709,827,719** | **707,821,867** | **100** |
| **1146002** | Ada ya Utunzaji Urithi | 1,200,000 | 0 | |
| **1422030** | Alama za Biashara | 350,700,000 | 231,263,078 | 66 |
| **1422031** | | 234,327,719 | 308,065,551 | 131 |
| **1422032** | Uandikishaji wa Majina ya Biashara | 72,400,000 | 85,570,898 | 118 |
| **1422034** | Ujira wa kutengeneza Nyaraka | 51,200,000 | 82,922,340 | 162 |
| | | | | |
| **R0107** | **Taasisi ya Viwango Zanzibar** | **976,000,000** | **175,000,000** | **18** |
| **1112008** | Malipo yatokanayo na Usimamizi wa Viwango | 976,000,000 | 175,000,000 | 18 |
| | | | | |
| **R0109** | **Tume ya Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji** | **250,000,000** | **48,874,000** | **20** |
| **1422077** | Malipo ya Kazi za Biashara | 250,000,000 | 48,874,000 | 20 |
| | | | | |
| **R0101** | **Ofisi Kuu Pemba** | **80,301,281** | **34,471,000** | **43** |
| **1422014** | Ukaguzi wa Mezani na Vipimo | 42,901,281 | 8,944,500 | 21 |
| **1422034** | Ujira wa Kutengeneza Nyaraka | 22,000,000 | 12,116,500 | 55 |
| **1422078** | Ukodishaji wa Maeneo Kibiashara | 12,000,000 | 13,410,000 | 112 |
| **1422031** | Uandikishaji wa Makampuni | 2,200,000 | 0 | |
| **1422032** | Uandikishaji wa Majina ya Biashara | 1,200,000 | 0 | |
| **Jumla Kuu** | | **2,367,797,000** | **1,068,147,198** | **45** |

***Chanzo: Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, 2021***

# Kiambatanisho namba 4:

## Matumizi ya Fedha kwa Kipindi cha Julai, 2020 – Machi, 2021

| S/N | Programu Kuu | Fedha Zilizotengwa Kwa Mwaka 2020 – 2021 TZS | Fedha Zilizopatikana kwa Kipindi cha (Julai- Machi, 2020/2021) TZS | Asilimia Ya Fedha Iliyopatikana |
|---|---|---|---|---|
| **PR01** | **Uendeshaji wa Uratibu wa Wizara ya Biashara** | **3,526,977,000** | **1,663,269,660** | **46** |
| | Utawala na Uendeshaji wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda | 2,294,967,000 | 1,035,143,826 | 45 |
| | Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti | 579,075,000 | 225,497,259 | 39 |
| | Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba | 652,935,000 | 372,628,575 | 57 |
| **PR02** | **Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali** | **12,782,152,000** | **836,401,472** | **7** |
| | Ukuzaji wa Viwanda | 3,612,751,000 | 811,240,472 | 22 |
| | Maendeleo ya Ujasiriamali | 9,169,401,000 | 25,161,000 | 0.3 |
| **PR03** | **Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara** | **3,316,771,000** | **1,267,740,871** | **38** |
| | Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji | 856,301,000 | 356,589,684 | 42 |
| | Ushindani Halali wa kibiashara na Kumlinda Mtumiaji | 376,870,000 | 131,207,227 | 35 |
| | Urahisishaji biashara na Ukuzaji Biashara za ndani | 1,215,900,000 | 427,229,000 | 35 |
| | Usajili wa Biashara na Mali | 867,700,000 | 352,714,960 | 41 |
| **PR04** | **Viwango na Tathmini ya Ubora** | **3,943,800,000** | **668,077,465** | **17** |
| | Viwango na Uthibiti Ubora | 3,943,800,000 | 668,077,465 | 17 |
| **JUMLA KUU** | | **23,569,700,000** | **4,405,489,468** | **19** |

***Chanzo: Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, 2021***

# Kiambatanisho namba 5:

## Mlinganisho wa Bei za Kuuzia Umeme Kati ya ZECO na TANESCO

| Maelezo | | ZECO | | | TANESCO | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **No.** | **Aina za wateja** | **Aina za Tarifu** | **Bei kwa Uniti (kWh)** | **Bei kwa Uniti (kVA)** | **Aina za Tarifu** | **Bei kwa Uniti (kWh)** | **Bei kwa Uniti (kVA)** |
| 1 | Lifeline | Z0 (1-50) | 79 | 0 | D1 | 100 (0-75), 350 (>75) | 0 |
| 2 | General Service | Z1 (1-1500) | 266 | 0 | T1 | 292 | 0 |
| 3 | Small Industries | Z2 (1-ALL) | 206 | 16,000.00 | T2 | 195 | 15,004.00 |
| 4 | Large Industries | Z3 (1-ALL) | 169 | 16,000.00 | T3(MV) | 157 | 13,200.00 |
| | | | | | T3 (HV-ZNZ) | 152 | 16,550.00 |

# Kiambatanisho namba 6:

## Huduma ya Ukaguzi

| Eneo la Ukaguzi | Jumla |
|---|---:|
| Uhakiki wa Mezani | 2,678 |
| Mita za Bohari (Airport na Mtoni) | 39 |
| Pampu za kuuzia mafuta | 317 |
| Magari ya kusambaza mafuta | 22 |
| Matangi ya mafuta | 30 |
| Uthibitisho wa tanks (Certification) | 3 |
| Uhakiki wa bidhaa zilizofungashwa | 35 |

***Chanzo: Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, 2021***

# Kiambatanisho namba 7:

## Uzalishaji wa Kiwanda cha Makonyo-Pemba kwa Mwaka 2020 - 2021

| Aina ya Mafuta | Lengo 2020/2021 (Kg) | Uzalishaji Halisi | Thamani (TZS) |
|---|---|---|---|
| Makonyo | 56,250.0 | 12,329.0 | 330,935,164.96 |
| Mdalasini | 75.0 | 100.50 | 32,662,500.0 |
| Mchaichai | 150.0 | 146.120 | 47,489,000.0 |
| Mrehani | 37.50 | 2.0 | 650,000.0 |
| Mkaratusi (Manukato) | 1,500.0 | 353.70 | 35,370,000.0 |
| Mkaratusi (Madawa) | 487.50 | 398.30 | 39,830,000.0 |
| Majani ya Mkarafuu | - | - | - |
| Majani ya Mkarafuu/Mgelema | - | 2,507.50 | 32,775,500.0 |
| Unga wa Karafuu | - | 3,519,50 | 205,516,332.56 |
| **JUMLA** | | | **725,228,497.52** |